SportPesa
TZS. 896,686,220
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**UGONJWA** wa saratani bado tishio nchini

UKURASA 3




UKURASA 11

Nipashe
Jumamosi Februari 5, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580847
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Rais Samia ashtuka polisi kujichunguza

**NI** kuhusu mauaji Mtwara, amtaka waziri kujitafakari, amwagiza Waziri Mkuu kuunda tume, atumbua wakurugenzi wanne halmashauri...*Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na wananchi wa wilaya ya Magu, mkoani Mwanza jana, alipokua njiani kwenda mkoani Mara. **PICHA: IKULU**

## Wabunge waibana serikali uwazi katika mikataba saba

UKURASA 4

## CCM yajivunia demokrasia na mtaji tril. 1.5/-

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA SC, MBEYA CITY MAJARIBUNI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya UBA, Gbenga Makinde (wa pili kushoto), kipata maelezo kuhusu uzalishaji wa magazeti kutoka Meneja wa Kiwanda cha Uchapishaji cha kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Balasubramaniyan Venkadachalam, alipotembelea ofisi za TGL, Mikocheni, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Rais Samia ashtuka polisi kujichunguza

**Na Waandishi Wetu,** MAGU

RAIS Samia Suluhu Hassan (pichani) ameshtukia kamati iliyoundwa na Jeshi la Polisi nchini kuchunguza mauaji yanayodaiwa kufanywa na askari wa jeshi hilo hivi karibuni mkoani Mtwara.

Amesema kuwa kwa mujibu wa taarifa alizonazo, mauaji hayo yamefanywa na Jeshi la Polisi, akimtaka Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni na Jeshi la Polisi kujitafakari.

Mkuu wa Nchi alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na wananchi wa Wilaya ya Magu mkoani Mwanza akiwa njiani kuelekea mkoani Mara kuhudhuria kilele cha maadhimisho ya miaka 45 ya kuzaliwa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Alimtaka Waziri Masauni kujitafakari na kuona kama kinachotokea kwa sasa dhidi ya raia ni sahihi, akisisitiza kuwa si sahihi polisi wahusike na mauaji hayo halafu waunde kamati kuchunguza tukio hilo.

Rais Samia alisema kuna mauaji yametokea Mtwara na kwa taarifa zilizopo Jeshi la Polisi ndilo lililofanya mauaji na kwamba taarifa alizonazo jeshi hilo limetengeneza kamati ya kufanya uchunguzi.

Alisema haiwezekani jeshi lifanye mauaji halafu hilo hilo lijichunguze lenyewe kisha lilete taarifa, hivyo akamwagiza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuunda kamati nyingine iende ikafanye uchunguzi wa mauaji yaliyofanywa na Jeshi la Polisi.

"Ndugu wananchi, tusubiri taarifa ya tume huru ya Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa, ituletee taarifa tuilinganishe na ya Jeshi la Polisi tuone taarifa hizo zinasemaje, tuchukue hatua mwafaka," alielekeza.

Rais Samia aliwaomba wananchi wadumishe amani na wasifanye mauaji badala yake wasaidie kuleta amani kwenye nchi ili kupata maendeleo.

Mwishoni mwa mwezi uliopita, askari polisi saba mkoani Mtwara walikamatwa kwa tuhuma za kufanya mauaji na kuutupa porini mwili wa mfanyabiashara wa madini mwenye umri wa miaka 25, huku mmoja wa watuhumiwa akidaiwa kujinyonga akiwa mahabusu ya polisi.

Kijana huyo aliyetajwa kwa jina la Mussa Hamisi, mkazi wa Wilaya ya Nachingwea mkoa jirani wa Lindi, anadaiwa kukamatwa na askari wa polisi Oktoba 20 mwaka jana akiwa katika nyumba ya kulala wageni mkoani Mtwara, akituhumiwa kwa wizi wa pikipiki na kufikishwa kituo cha polisi kwa ajili ya mahojiano.

Inadaiwa kuwa baada ya kuhojiwa, alibainika kuwa na fedha zipatazo Sh. milioni 2.5 na kutaja kiasi kingine ambacho alikihifadhi nyumbani kwao wilayani Nachingwea mkoani Lindi, ambako maofisa hao walifunga safari hadi wilayani humo katika nyumba ya wazazi wake kupekua na kubaini kuwapo dola za Marekani 13,500 na kuondoka nazo wakiwa wamemweka chini ya ulinzi.

Hawa Bakari, mama mzazi wa kijana huyo, aliiambia Nipashe mwishoni mwa mwezi uliopita kuwa mara ya mwisho kuonekana machoni mwa ndugu zake, kijana wake ni Januari 5



mwaka huu huku akieleza namna askari polisi walivyofika nyumbani kwao kwa ajili ya kuchukua fedha alizokuwa nazo.

**RIPOTI YA NIPASHE**

Kwa siku tatu mfululizo kuanzia Desemba 20 hadi 22 mwaka jana, Nipashe ilichapisha ripoti maalumu iliyokuwa na kichwa cha habari kilichosomeka 'Kitendawili cha usalama mahabusi walioko polisi', ikifichua namna watuhumiwa wanavyopoteza maisha wakiwa mikononi mwa askari polisi kutokana na vipigo na madhila mengine.

Ndani ya ripoti hiyo, wadau wa sheria na haki za binadamu, akiwamo Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Anna Henga, walikosoa kitendo cha polisi kujichunguza kwa tuhuma zinazowakabili.

# ... Atumbua wakurugenzi wanne akiwa njiani

**Na Mary Geofrey**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametengua uteuzi wa wakurugenzi watendaji wa halmashauri nne akiwa safarini kuelekea mkoani Mara kutokana na matumizi mabaya ya fedha za mkopo uliotolewa kwa ajili ya kukabiliana na athari za ugonjwa wa UVIKO-19.

Waliokumbwa na rungu hilo ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa, Mkurugenzi wa Manispaa ya Iringa, Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya na Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida Mjini.

Rais Samia pia amemweka kiporo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Geita ambaye uchunguzi dhidi yake bado unaendelea.

Rais Samia alitangaza uamuzi huo jana wakati akiwa njiani wilayani Magu mkoani Mwanza, akielekea mkoani Mara kwa ajili ya kilele cha maadhimisho ya miaka 45 ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) yanayofanyika leo.

"Siku ile tunazitangaza fedha nilisema kama mkurugenzi anataka kuona rangi yangu halisi achezee hizo fedha, sasa kwa taarifa zilizopo, Buchosa, Iringa, Mbeya na Singida Mjini wakurugenzi wamechezea fedha. Mheshimiwa Waziri, wakurugenzi hao nimewatengua sasa hivi," alisema.

Rais Samia aliongeza: "Nimewatengua sasa hivi na baadaye nitaona ripoti yako inasema nini maana mna kawaida ya kuwafichiafichia lakini nina ripoti kabla ya kwenu. Hawa wakurugenzi nimewatengua sasa hivi.

"Yule wa Geita endeleeni na uchunguzi na mimi timu yangu iko pale inafanya uchunguzi, naye wakiniletea ana makosa kama haya, na yeye atatenguliwa. Kwa hiyo wale wanne nimewatengua, wa Geita ninasubiri timu yangu inipe taarifa."

Awali Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alisema wizara hiyo ilipata taarifa za ubadhirifu kutoka kwa Mkuu wa Mkoa kuhusu Wilaya ya Buchosa na maeneo mengine.

Alisema TAMISEMI pia inafanya uchunguzi kuhusu kushuka kwa mapato ya nusu mwaka ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya kutokana na upotevu mkubwa wa mapato.

Waziri huyo alisema uchunguzi wa awali ulionyesha kuna mashine za posi 72 zilizimwa kwa siku zaidi ya 100 na wanaendelea kufanya uchunguzi ili kubaini sababu na kwamba tayari wameshaunda kamati.

Bashungwa pia alibainisha kuwa wanaendelea kuchunguza Halmashuari ya Geita Vijijini baada ya Mbunge wa Jimbo hilo, Joseph Musukuma, kueleza kuwapo ubadhirifu na wanaendelea na uchunguzi kwa mujibu wa taratibu za wizara hiyo.

Alisema pia walifanya uchunguzi kwa Halmashauri za Singida na Iringa Mjini na wanaendelea kufanya tathmini ya matumizi ya fedha zinazotolewa na serikali.

"Ulielekeza hutataka kusikia hata senti moja imeibiwa au imetumiwa vibaya nje ya maelekezo ya serikali na nikuhakikishie Mheshimiwa Rais, maelekezo yako tunayasimamia na wale wanaoenda kinyume cha taratibu tutakuwa tunakuletea taarifa ili uchukue hatua," alisema Bashungwa.

Baada ya kumaliza kutoa taarifa hiyo, ndipo Rais Samia alipomwagiza Waziri Bashungwa kutaja maeneo mengine ambayo kumefanyika ubadhirifu kisha akachukua hatua.

HABARI KITAIFA

# Wagonjwa wapya wa saratani tishio

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TATIZO la saratani nchini limetajwa kuongezeka kwa kasi, ikibainishwa kuwapo wagonjwa wapya 42,060 kwa mwaka huku 28,610, sawa na asilimia 68 hufariki dunia kutokana na ugonjwa huo.

Taarifa za mwaka 2021 za Taasisi ya Saratani Ocean Road zinaonyesha saratani zinazoongoza kwa wanaume ni tezi dume huku wanawake ni ya mlango wa kizazi.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliyasema hayo jana jijini hapa alipotoa tamko la Siku ya Saratani Duniani.

Alisema kuwa katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, Tanzania imeshuhudia ongezeko kubwa la wagonjwa wa saratani zinazochangiwa na mtindo wa maisha kulinganishwa na ilivyokuwa awali ambapo wagonjwa wengi walikuwa ni wale wenye saratani zinazotokana na maambukizi ya virusi.

Alisema takwimu za Shirika la Umoja wa Mataifa la Utafiti wa Saratani (IARC) za mwaka 2018 zinaonyesha kwa Tanzania watu 76 kati ya 100,000 hugundulika kuwa na saratani.

"Takwimu kutoka kwenye kanzidata (Population Based Cancer Registry) zilizoanzishwa kwa kanda, zinaonyesha kwamba wagonjwa wapya 14,136 walifikiwa na huduma ambayo ni sawa na asilimia 33 ya makadirio ya wagonjwa wapya wote kwa mwaka 2021, ikiwa ni ongezeko la asilimia tano kulinganisha na takwimu za mwaka 2020 ambapo jumla ya wagonjwa wapya 12,096, sawa na asilimia 28 walionwa,"alisema.

Alibainisha kwa wanaume saratani zinazowaathiri zaidi ni pamoja na tezi dume kwa asilimia 21, saratani ya koo (asilimia 11.8), saratani ya utumbo mkubwa na mdogo (asilimia tisa) na saratani ya mdomo na kinywa (asilimia 7.3).

"Tezi dume inaongezeka sana, nitoe wito kwa wanaume mjitokeze kupima, acheni kuogopa. Kwa sasa kuna kipimo cha kisasa sio kile ambacho mnakijua au kukifikiria... Na pia kwa wanawake mkijitokeza kupima saratani ya mlango wa kizazi na matiti, tutaweza kudhibiti kwa kiwango kikubwa," alisema.

Waziri huyo alisema kwa wanawake saratani zinazowaathiri zaidi ni pamoja na saratani ya mlango ya kizazi (asilimia 43), saratani ya matiti (asilimia 14.2) na saratani ya koo (asilimia 3.8).

Hata hivyo, alitaja sababu nyingine ya ongezeko la wagonjwa hao na magonjwa mengine yasiyoambukiza linachangiwa na matumizi ya tumbaku na bidhaa zake, matumizi ya pombe kupita kiasi na ulaji usiofaa kama kutokula mbogamboga na matunda, matumizi ya chumvi na sukari kwa wingi.

Kutokana na hali hiyo, Waziri Ummy aliagiza itengwe siku maalum kila mwezi kwa ajili ya kupima saratani kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na uchunguzi.

Pia alisema katika kuongeza uelewa kwa jamii, serikali inaandaa mtaala wa mafunzo shuleni unaozungumzia magonjwa hayo na udhibiti wake.

"Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikifanya kampeni maalum na kuhimiza wananchi kufanya uchunguzi wa afya zao ili kubaini ugonjwa katika hatua za awali," alisema.



Diwani wa Kata ya Kivukoni, jijini Dar es Salaam, Sharik Choughule (kulia), akikaanga samaki katika Soko la Feri jana, baada ya kuwakabidhi wakaanga samaki majiko mapya ya kisasa 48. Wa (tatu kushoto) ni Mkuu wa Soko hilo, Dennis Mrema. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# CCM yajivunia mtaji trilioni 1.5/-

**Na Beatrice Shayo,** MUSOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimetaja mambo kinayojivuania katika kuadhimisha miaka 45 ya chama ikiwa ni pamoja na kuimarisha demokrasia, kuimarisha umoja wa taifa, kuimarika kwa Muungano na kina mtaji wa Sh. trilioni 1.5.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC ) ya CCM Itikadi na Uenezi Shaka Hamdu Shaka, alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari makao makuu ya chama hicho Mkoa wa Mara wakati akielezea mafanikio mbalimbali yaliyopatikana nchini kutokana na chama hicho.

Alisema chama hicho kimeendelea na harakati za kaleta maendeleo nchini na kudumumisha amani na muungano kutokana na juhudi za makusudi za chama hicho katika kutatua vikwazo vya Muungano kwa maslahi mapana ya Watanzania.

"Moja ya mafanikio makubwa yaliyopatikana ni kudumu na kuimarika kwa muungano wetu. Katika kipindi cha miaka 45 iliyopita Muungano wetu umezidi kuimarika kutokana na juhudi za makusudi za chama chetu za kuhakikisha kuwa muungano wetu unadumu milele," alisema

Alisema CCM ndani ya miaka 45 imefanikiwa kusimamia muundo wa sera, mikakati na aina ya siasa inayohitajika katika nyakati za sasa jambo lililosaidia kulinda na kusimamia usalama wa taifa na watu wake ili kudumisha amani, umoja na kujivunia uhuru wake.

Shaka alisema kazi kubwa ya utekelezaji wa sera kwa miaka yote ya utawala wa CCM madarakani ni kuhakikisha umoja wa kitaifa unadumu na kubaki, kupinga siasa chafu za ukabila, rangi, dini au ukanda badala yake sera zake zimekuwa zikihimiza umoja na mshikamano, hali ambayo imelifanya taifa kuwa lenye utulivu, upendo na ushirikiano.

"Katika nyakati zote kila mwananchi amekuwa mlinzi wa taifa lake, askari wa mstari wa mbele anayehakikisha hatokei adui akayejivisha koti la kuwa kibaraka au wakala, badala yake mapambano yameelekezwa dhidi ya maadui ujinga, umaskini na maradhi," alisema.

Shaka alisema lengo kuu la CCM kilichozaliwa Februari 5, mwaka 1977 kutokana na ridhaa ya wanachama wa vyama viwili, lilikuwa ni kuongoza Watanzania katika mapambano magumu ya kudumisha na kuimarisha uhuru wa nchi na kila Mtanzania.

Alisema CCM ilikuwa na jukumu kubwa la kulitoa taifa na watu wake kwenye unyonge na umaskini na kuwa nyuma kimaendeleo.

"Bahati nzuri kwa muda wote wananchi wameonyesha imani kubwa kwa chama chetu kwa kuendelea kukichagua na kukipa heshima ya kuliongoza taifa letu," alisema Shaka.

"Muungano wetu ni mfano bora wa kuigwa siyo tu barani Afrika bali duniani kote. Watanzania tumeudhihirishia ulimwengu kuwa dhamira yetu ya kuungana ni imara na haitetereki.

"Tutaendelea kuimarisha muungano wetu kwa faida ya nchi yetu na watu wetu tunafanya hivyo kwa kutambua faida kubwa na nyingi zinazotokana na muungano wetu," alisema Shaka

# Waonywa upandishaji bei za vifaa vya ujenzi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Prof. Godius Kahyarara, amewaonya wasambazaji wa bidhaa za vifaa vya ujenzi kupandisha bei hivyo kuwaumiza wananchi.

Amesema kupandisha bei za bidhaa hizo bila sababu ya msingi ni kosa kisheria na atakayebainika kufanya hivyo, atachukuliwa hatua. Prof. Kahyarara aliyasema hayo juzi alipokutana na kuzungumza na wasambazaji wa bidhaa za vifaa vya ujenzi Dodoma, kuhusu sababu za upandishaji wa bei na kupokea maoni ya jinsi ya kukabiliana na suala hilo.

Lengo la kikao hicho ni kukuza biashara na kuwalinda watumiaji wa bidhaa pamoja na kutimiza lengo la serikali katika kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya taifa na wananchi.

Katibu Mkuu huyo, aliwashauri wafanyabiashara na wasambazaji hao kujiandaa na kufanya biashara kwa ushindani pamoja na kuchangamkia fursa za Mkataba wa Kuanzisha Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) ambao Tanzania imeridhia na kujiunga.

Mkataba huo unalenga kuwezesha uwekezaji na ufanyaji biashara baina ya nchi na nchi katika soko lenye watu takribani bilioni 1.3 linalotarajiwa kuleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi, kibiashara na kijamii barani Afrika. Nao wasambazaji wa bidhaa za ujenzi husuan saruji, nondo na mabati jijini Dodoma, walipata fursa ya kutoa sababu zinazochangia kupanda kwa bei ya bidhaa hizo ikiwamo kununua bidhaa kwa bei kubwa kutoka kwa wasambazaji wakubwa.

Walizitaja sababu zingine kuwa ni gharama kubwa za usafirishaji wa bidhaa hizo kutoka viwandani hadi maeneo husika pamoja na kupanda kwa bei ya malighafi za kutengenezea mabati kutoka nje ya nchi pamoja na gharama kubwa za kusafirisha malighafi kutoka nje ya nchi.

Kuhusu namna ya kukabiliana na upandaji wa bei za vifaa vya ujenzi, wasambazaji hao waliishauri serikali kuanzisha mfumo wa bei elekezi ya saruji kulingana na maeneo waliyopo kijiografia.

Pia waliomba serikali kuwashauri wamiliki wa viwanda kuboresha mfumo wa usambazaji wa bidhaa kwa kuruhusu kuwa na wasambazaji wa bidhaa wengi badala ya kuwa na wasambazaji wakubwa wachache.


KUMBUKUMBU




MRS:VERDIANA K ALLY

Ilikua tarehe 5/2/1996 tangu ulipotutoka mpendwa wetu, ni miaka 26 sasa mama yetu Mrs VERDIANA K ALLY na kutuachia pengo lisilozibika, ingawa kimwili haupo nasi lakini kiroho upo nasi

Tunathamini mchango wako katika familia upendo,busara na ukarimu.Daima unakumbukwa na ,watoto wako ALEX na MARIETHA pamoja na wajukuu VERDIANA, VIVIAN, ALLEN, LEGAL, STACY, VALENTINE, AUBREY, ALVIN, ALEXANDER, VOILANDA pamoja na JAYDEN.

Tulikupenda sana lakini mwenyezi Mungu alikupenda zaidi.
BWANA AMETOA BWANA AMETWAA JINA LAKE LIHIMIDIWE AMEN.

166895



Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, Mosses Mzuna (kulia), akiwasikiliza baadhi ya wazee wenye ulemavu wa ukoma kwenye kituo chao wanacholelewa cha Maji ya Chai, Wilayani Arumeru, mkoani Arusha, wakati wafanyakazi wa Mahakama hiyo na wadau wa Haki jinai na madai, walipotembelea kituo hicho juzi, kwenye hitimisho la wiki ya sheria na kutoa msaada wa vyakula na vitu mbalimbali. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Wabunge waibana serikali uwazi katika mikataba saba

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

WABUNGE wa Bunda, Boniphace Getere na Ndanda, Cecil Mwambe (wote CCM), wameitaka serikali ipeleke bungeni mikataba saba ili wabunge waisome na kuwa na uelewa wa kina kuishauri serikali.

Mikataba hiyo ni ya migodi ya madini, ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), Bandari ya Bagamoyo, gesi Mtwara, ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, Bomba la Mafuta na stempu za kielektroniki.

Katika swali la msingi, Mbunge Mwita alihoji ni lini serikali itawasilisha mikataba hiyo bungeni ili wabunge waifahamu, huku katika swali la nyongeza Mwambe akisema ni muhimu mikataba hiyo ikafikishwa kwenye chombo hicho ili waishauri vyema serikali.

Mbunge Mwita pia alitaka kujua ni mikataba mingapi kati ya hiyo imewahi kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG).

Akijibu swali la msingi, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geophrey Pinda, alisema taarifa za mikataba ya SGR, ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, migodi ya madini, Bomba la Mafuta na mradi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam kwa nyakati tofauti, taasisi na mashirika yanayoisimamia yamekuwa yakiwasilisha kwenye Kamati za Kudumu za Bunge taarifa za mikataba ya miradi hiyo.

Alisema kamati zina mamlaka kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge kupata taarifa zozote kuhusiana na mikataba ya miradi.

"Miradi hii imekuwa ikikaguliwa na CAG. Kwa kuwa baadhi ya miradi serikali inamiliki kwa asilimia 100 na mingine ni mbia, hivyo taarifa zake huwasilishwa katika Bunge lako tukufu kupitia ripoti ya CAG," alifafanua.

Naibu waziri huyo alisema katika bajeti ya mwaka 2019/20, kuna taarifa ya kina ya mradi wa SGR na Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere, na kwamba mradi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam umekuwa ukifanyiwa ukaguzi wa kawaida kila mwaka.

"Nipende kumwarifu mbunge na pia Bunge lako tukufu kuwa Bunge limekuwa likipokea taarifa za mikataba na ripoti za CAG," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mwambe alisema mwaka jana mwishoni, Spika aliunda Kamati ya Viwanda na Biashara na Kamati ya Bajeti, ambazo zilikutana kwa nia ya kutaka kupitia mambo mbalimbali ikiwamo malalamiko ya wafanyabiashara kuhusu bei kubwa ya stempu za kielektroniki.

"Pamoja na mazungumzo yale serikali na Mamlaka ya Mapato (TRA), waliendelea kusaini mkataba wa kinyonyaji kwa wananchi, Je, (waziri) yupo tayari kuleta mkataba wa kampuni ya SCIPA (stempu za kielektroniki) na serikali unaohusisha na masuala ya stempu za kielektroniki?" Mwambe alihoji.

Pia alisema wabunge ambao siyo wajumbe wa kamati husika, ni muhimu wakaona na kusoma mikataba hiyo ili waishauri serikali.

Akijibu swali hilo, naibu waziri huyo alisema: "Kwa hili linalohusu stempu tutafanya mawasiliano na taasisi inayohusika ili tuweke sawa katika hili eneo lililoonyesha shaka.

"Kuhusu suala la kuwasilisha mikataba katika Bunge lako tukufu, mikataba hii huwa inapita kwenye kamati zilizowekwa na kama Bunge litataka mkataba ufikishwe mbele ya Bunge lote, basi uamuzi unatoka kwenye kamati baada ya kupitia taarifa zinazowasilishwa."

# Mlalamikaji kesi ya kina Mbowe atajwa

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI wa 13 wa upande wa Jamhuri, Inspekta Tumaini Swila, amedai kuwa wakati anafungua jalada la kula njama kufanya uhalifu, mlalamikaji alikuwa Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai nchini, Kamishna wa Polisi Robert Boaz na mlalamikiwa Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe.

Inspekta Swila alidai hayo jana Mahakama Kuu, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joackim Tiganga wakati akiongozwa kutoa ushahidi na Wakili wa Serikali, Robert Kidando.

Akitoa ushahidi, alidai ni mkaguzi wa polisi, yuko Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Kipolisi Temeke na anafanya kazi ya upelelezi kwa miaka 24 sasa.

Alidai alikuwa katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI) Julai 14 mwaka 2020, alimkuta DCI, Kamishna Boaz na Kamishna Msaidiz wa Polisi, Ramadhan Kingai.

Shahidi alidai kupokea maelekezo kutoka kwa Afande Kingai kuwa anatakiwa kufungua jalada la uchunguzi, DCI alipokea taarifa kutoka kwa Luteni Urio juu ya uwapo wa kundi linaloratibiwa na Mbowe kufanya uhalifu.

Alidai kundi hilo linaratibiwa kulipua vituo vya mafuta, kuchoma moto masoko, kukata miti kwenye barabara kuu ili kuzuia magari, kuwadhuru viongozi mbalimbali wa serikali kwa lengo la kuleta taharuki.

"Afande Kingai alitaka nifungue jalada la uchunguzi nilifungua, wakati ninafungua mlalamikaji alikuwa Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai nchini, Kamishna Robert Boaz na mlalamikiwa Freeman Mbowe.

"Nilifungua jalada la kutaka kufanya vitendo vya uhalifu, Kingai aliniambia nilihifadhi atanipa maelekezo, Julai 15 mwaka 2020, Kamishna Boaz alitaka nimsaidie Afande Kingai kufanya upelelezi," alidai shahidi huyo.

Alidai Kingai alimfahamisha kwamba Luteni Urio alishawapata vijana wa kuwapeleka kwa Mbowe na alimtaka afungue jalada la kesi Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam.

Shahidi alidai alifungua jalada la kula njama kati ya Mei na Julai mwaka 2020 na kwamba kuna kundi la watu wanapanga kufanya vitendo vya kigaidi katika mikoa mbalimbali nchini.

"Afande Kingai alitaka nisiandike jina la mtuhumiwa Mbowe katika taarifa hiyo ili kuepusha uvujaji wa taarifa, jina lake lingekuwapo kwenye taarifa angeweza kujua na kusitisha utekelezaji aliokuwa kapanga kufanya na wenzake.

"Agosti 6 mwaka 2020, Afande Kingai alinipigia simu akaniambia kuna watuhumiwa wawili wamekamatwa Moshi, Agosti 7 niliitwa Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam, nilipofika niliwakuta kina Afande Kingai nje," alidai.

Alidai kuwa alipokea simu za washtakiwa kutoka kwa Koplo Goodluck Minja, alikabidhiwa maelezo ya mashahidi, hati ya kukamata mali lakini watuhumiwa hakuwaona.

Shahidi alidai Afande Kingai alimkabidhi maelezo ya onyo ya Adamu Kasekwa na Afande Jumanne alimkabidhi maelezo ya onyo ya Mohammed Ling'wenya ambapo vitu vyote alivyokabidhiwa alihifadhi katika kabati la chuma lililopo Makao Makuu ndogo ya Upelelezi Dar ea Salaam.

Shahidi huyo alidai kuwa Agosti 8, 2020 waliwahamisha watuhumiwa, Kasekwa na Ling'wenya kutoka Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam na kuwapeleka Kituo cha Polisi Mbweni, Afande Jumanne akawakabidhi chumba cha mashtaka kisha wakaondoka.

Inspekta Swila alidai alionana na Luteni Urio ofisini kwake Agosti 11, 2020 na alichukua maelezo yake, akieleza mawasiliano yake na Mbowe kupitia mtandao wa telegram.

Alidai Urio alitaja namba walizokuwa wakiwasiliana za Mbowe 0719 933386, 0784 779944 na namba za Luteni Urio 0787 555200 na 0754 612518.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Halfani Bwire, Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya ambao wanakabiliwa na mashtaka sita yakiwamo ya kula njama kufanya vitendo vya kigaidi.

## HABARI KITAIFA

# RC apigia debe chanjo UVIKO- 19

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, amewasisitiza wananchi mkoani hapa kujitokeza kupata chanjo ya UVIKO-19 ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona na kutopata madhara makubwa pindi wanapokumbwa nao.

Mjema alitoa rai hiyo juzi kwenye kikao cha kujenga uelewa kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini chini ya mfuko wa maendeleo ya Jamii (TASAF), tathimini ya lishe na utoaji wa huduma za chanjo ikiwamo ya UVIKO-19.

Alisema mkoa huo ulipokea dozi za 151,971 za chanjo ya UVIKO- 19 na mpaka sasa zimeshatumika dozi 113,121 sawa na asilimia 74.4, hivyo kuwataka wananchi wajitokeze kwa wingi kupata chanjo ili kujilinda na ugonjwa huo.

"Nawaomba viongozi wote wakiwamo wakuu wa wilaya na waratibu wa chanjo, tuendelee kushirikiana kutoa elimu kwa wananchi na kuwasisitiza wajitokeze kwa wingi kupata chanjo ya UVIKO-19. Wale ambao wamepata dozi ya kwanza warudi kupata dozi ya pili," alisema Mjema.

Kuhusu TASAF, alisema tangu Julai, 2015 hadi Desemba, mwaka jana, mkoa ulipokea Sh. bilioni 37.3 kwa ajili ya malipo kwa walengwa wapatao 45.487 na kwamba kumekuwa na mafanikio kwenye utekelezaji wa mpango huo kutokana na kaya 24,600 kujiunga na Bima ya Afya (CHF) iliyoboreshwa.

# Mauaji mengine yaibuka Dar, Njombe

**Mauaji mengine yaibuka Dar,** NJOMBE

WIMBI la mauaji ya watu limeendelea kutikisa nchi, huku safari hii ikiripotiwa kutokea kwa matukio ya watu watano kuuawa katika mikoa ya Dar es Salaam na Njombe.

Mkoani Dar es Salaam, Yunge Maduhu (18), mfanyakazi wa ndani na mkazi wa Kimara Suka, mtaa wa Bwawani, alikutwa amepoteza maisha Februari 2 mwaka huu, huku utata ukitawala kutokana na sababu ya kifo hicho kutojulikana.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema msichana huyo alikutwa amelazwa chini huku akiwa amefunikwa taulo katika baadhi ya sehemu za mwili wake.

"Ni kweli tuna taarifa za kifo cha binti huyo lakini bado kina utata. Hatujajua kuwa kauawa au ni kifo cha kawaida kwa kuwa hakukutwa na jeraha la kukatwa na kisu wala panga mwilini mwake. Lakini kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama tunaendelea kufanya uchunguzi.

"Baada ya uchunguzi, endapo itabainika kuwa kauawa, Jeshi la Polisi litawatafuta watuhumiwa na kuwafikisha katika vyombo vya usalama na hatua zaidi za kisheria zitachukuliwa dhidi yao," alisema Muliro.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Bwawani, Anastazia Mtutuma, alisema Februari 2, majira ya alasiri, akiwa nyumbani kwake, aliitwa na msichana wa jirani ambaye alikuwa anaishi karibu na Yunge na alipofika alikuta Yunge amelala chini akiwa amefunikwa na taulo sehemu ya mwili na kichwani.

"Nikiwa na mama mwenye hii nyumba pamoja na baadhi ya majirani niliifunua taulo kichwani kwa huyo binti ili kuona kama tunaweza kumpatia huduma ya kwanza lakini baada ya kumfunua niligundua hayupo kwenye hali ya kawaida, ndipo tukawapigia polisi," alisema Anastazia.

Alisema alimgusa binti huyo miguuni kwa lengo la kumsitiri kwa kuwa baadhi ya nguo zake zinazosadikika kuwa alikuwa amezivaa zilikuwa zimetupwa pembeni zikiwamo za ndani.

Regina Mshokela ambaye ni mama aliyekuwa akiishi na binti huyo tangu mwaka 2019, alisema hakuwa na tatizo lolote. Alisema siku ya tukio alikuwa njiani akitoka kazini ndipo alipopigiwa simu na mwalimu kutoka shuleni anakosoma mtoto wake akimwarifu kuwa dereva amemrudisha mtoto nyumbani lakini hakukuwa na mtu wa kumpokea.

"Niliporudi nyumbani nilikuta geti limefungwa nikafungua na kuingia ndani, nilikuta vitu vimetupwa tupwa pia kulikuwa na harufu kali kama ya marashi nikaamua kutoka nje," alisema Regina.

Licha ya kifo cha msichana huyo, alisema ndani ya nyumba hiyo kuna baadhi ya vitu viliibwa vikiwamo televisheni, pasi, begi na mchele kilo 10.

**WANNE NJOMBE**

Kutoka Njombe, watu wanne wameripotiwa kuuwawa katika matukio matatu tofauti, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, amethibitisha.

Kamanda Issa alisema katika tukio la kwanza Israel Msigwa (39) maarufu kama mtoa roho, anadaiwa kumuua mtoto wake Haskad Msigwa (7), mwanafunzi wa darasa la awali Shule ya Msingi Kilimahewa, Halmashauri ya Mji Makambako kwa madai ya kukojoa kitandani.

Alisema tukio hilo lilitokea Januari 24, mwaka huu, majira ya saa 11:00 kwa madai kwamba mtuhumiwa alimpiga mtoto huyo kwa fimbo na waya mweusi wa umeme sehemu mbalimbali za mwili.

Mtuhumiwa baada ya kutenda jambo hilo, Kamanda alisema alikimbia na kukamatwa maeneo ya kijiji cha Kilosa, Mufindi mkoani Iringa.

Kamanda alisema tukio la pili lilitokea Imalilo wilayani Wanging'ombe kwa Ambwene Sanga (34) kudaiwa kumuua mwanawe wa kambo, Mesia Kaduma (5) mwanafunzi wa chekechea Shule ya Msingi Imalilo kwa kumkatakata mapanga sehemu mbalimbali na kumficha korongoni.

Issah alimtaja mtuhumiwa mwingine ambaye anadaiwa kushurikiana na baba huyo wa kambo kufanya mauaji hayo kuwa ni Michael Mbilinyi (32).

Katika tukio la tatu, alisema watu wanne akiwamo mganga wa jadi, Joseph Mginda (41) mkazi wa Sovi, Makambako, wanashikiliwa na polisi kwa tuhuma za kuwaua Suzani Mtitu (38) na Kasimu Kimkanga (35) na kuwatupa kwenye msitu wa kupandwa wa TANWAT mjini Njombe.

Aliwataja watuhumiwa wengine kuwa ni Andrea Valowoka (45), Gadi Mwanzalila (36) rafiki wa mganga na Kelvin Mabena (29) dereva aliyebeba miili ya marehemu.

Kamanda alisema tukio hilo lilitokea Januari 11, mwaka huu, majira ya saa 7:00 mchana na kwamba watuhumiwa walifanya hivyo kwa madai ya kutaka utajiri.

● **Imeandikwa na Maulid Mmbaga, DAR na Elizabeth John, NJOMBE.**


## NOTISI/TANGAZO

**MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD,MBUZAX AUCTION MART** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| ARUSHA | SIRILI PANTALEO MATERU | NYUMBA YENYE HATI NO.18996 KIWANJA No.797 KITALU 'HH' THEMI NA KIWANJA CHENYE MSINGI HATI NO.34242 KIWANJA No.117 KITALU 'J' NJIRO | CYRIL PANTALEO MATERU NA SIRILI PANTALEO MATERU | NYUMBA IPO THEMI NA KIWANJA KIPO NJIRO - ARUSHA | 23/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | JAMES PATRICK MUSHI | NYUMBA YENYE HATI NO.32899 KIWANJA NO.520 KITALU 'JJ' OLORIEN MUSHONO | JAMES PATRICK MUSHI | OLORIEN MUSHONO | 22/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | UYACODE VICOBA PROGRAM | LESENI YA MAKAZI KNDO 29299-KND/MBR/MWZ/10/2 | UYACODE VICOBA PROGRAM HQ | MAKUBURI UBUNGO | 23/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | EVA JAMES MBELE | NYUMBA | EVA JAMES MBELE | CHANIKA | 22/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | MARIAM THADEI HAULE | NYUMBA | MARIAM THADEI HAULE | KIMARA B | 23/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | MARY MEDARD SILAYO | NYUMBA | MARY MEDARD SILAYO | MLONGANZILA | 24/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KINONDONI | GLORY SIMON MINJA | NYUMBA | GLORY SIMON MINJA | TABATA BARAKUDA | 25/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | UPENDO JOSEPH CHALAMBO | NYUMBA | UPENDO JOSEPH CHALAMBO | KIMARA BONYOKWA | 01/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | FATUMA ISSA SHIDA | NYUMBA | JUMA SHIGONGO | KIWANGWA | 28/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | LEAH JOHN MPAPALIKA | NYUMBA | LEAH JOHN MPAPALIKA | KIMARA-STOPOVER | 23/02/2022 SAA 4;30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | CHRISTOPHER BERNAD KASWALALA | NYUMBA | CHRISTOPHER BERNAD KASWALALA | MALAMBA MAWILI-MSIGANI | 23/02/2022 SAA 7:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| UBUNGO | GERALD VENANCE SALLEH | NYUMBA | GERALD VENANCE SALLEH | MBEZI LUIS | 25/02/2022 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | WANSAGULA MOSES NATUMWA | NYUMBA | PILI HARUNA BUHANGWA | KINYAMWEZI- PUGU | 02/03/2022 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | NAHAL ALLY LIPWAI | NYUMBA | NAHAL ALLY LIPWAI | KONGOWE | 02/03/2022 SAA 7:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| UBUNGO | JOHN WILLIUM GUIDO | NYUMBA | JOHN WILLIUM GUIDO | KIBAMBA MLOGANZIRA | 24/02//2022 SAA 7:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| UBUNGO | BELU NURSERY AND PRIMARY SCHOOL | NYUMBA | BERNAD E.KIHIYO AND LUCY L. KIHIYO | TANDALE SOKONI | 25/02/2022 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | GEORGE JAPHET NDENGA | NYUMBA | GEORGE JAPHET NDENGA | KINYEREZI | 28/02/2022 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | JAMILA KONDO GEMA | NYUMBA | JAMILA KONDO GEMA | KIPAWA- KIPUNGUNI | 22/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | TABU JANETH JULIUS SEDA | NYUMBA | BRAITI SANGA | MAJOHE MJI MPYA | 22/02/2022 SAA07:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| UKONGA | ABDULHMAN RAJABU MAHABA | NYUMBA | ABDULHMAN RAJABU MAHABA | ZINGIZIWA | 24/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | MARIANA PATRICK SEDA | NYUMBA | MAILABE MICHAEL BINA | PUGU-KINYAMWEZI | 24/02/2022 SAA07:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| UBUNGO | MWANAHAMISI KONDO MATAMBO` | NYUMBA | MWANAHAMISI KONDO MATAMBO | RUVU DARAJANI | 21/02/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | EMMANUEL WILLIAM NNKO | NYUMBA | EDWARD MATHEO OLOMI | MTAA WA LUHANGA,ILALA | 22/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | ADON FOCUS MAUKI | NYUMBA | ADONI FOCUS MAUKI | MTAA WA MZINGA 'A' TEMEKE | 22/02/2022 SAA07:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| AGGREY | GAUDENCIA MATHIAS TEMBA | NYUMBA | GAUDENCIA MATHIAS TEMBA | MTAA WA PUGU STATION,ILALA | 24/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | EDMUND KAJUNGU MENDRAD | NYUMBA | EDMUND KAJUNGU MENDRAD | KILOLELI - MWANZA | 24/02/2022 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | RWEYEMAMU MENDRAD KABENDERA | NYUMBA | RWEYEMAMU MENDRAD KABENDERA | NYASHISHI MWANZA | 28/02/2022 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | GRACE BARNABAS MASUKA | NYUMBA | GRACE BARNABAS MASUKA | USAGARA-MWANZA | 25/02/2022 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |

MASHARTI YA MNADA

| | |
|---|---|
| 1 | Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba au Kiwanja ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14. |
| 2 | Ikiwamnunuziatashindwakutimizashartilolote la mnada kuhusiana na malipo yaawali,hatarudishiwapesayoyotealiyokwishailipa. |
| 3 | Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0759648448/0714939933/0718038313/0768672367/0754497396 |
| 4 | Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote. |

166918

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kozi za FIFA, UEFA, TFF zilete mabadiliko nchini

**KATIKA** kuhakikisha mpira wa miguu hapa nchini unakuwa na maendeleo, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa kushirikiana na mashirikishiko ya kimataifa ambayo ni FIFA, UEFA na CAF, wanaendesha kozi na mafunzo mbalimbali hapa nchini.

Mafunzo na kozi hizo zinazofanyika hapa nchini ni za utawala, uamuzi na ukocha katika ngazi mbalimbali.

Tofauti na miaka ya nyuma, tangu uongozi wa Rais wa TFF, Wallace Karia, tumeshuhudia kozi hizo zikifanyika kwa kuleta wakufunzi wa kimataifa kutoka FIFA, UEFA na CAF ili kuwapa elimu stahiki inayotakiwa wadau wanaohusika katika nafasi hizo.

Lengo la TFF kuratibu mafunzo hayo ni kutaka kuona kila mdau katika eneo lake anafanya majukumu yake kwa weledi na hatimaye kupandisha kiwango cha wachezaji wa soka wa Tanzania.

Msingi mwingine wa mafunzo hayo si tu kuboresha uwezo wa wasimamizi hawa wa shughuli za uendeshaji mpira wa miguu kila siku, lakini ni kutaka kuona kasi ya maendeleo ya wadau hawa muhimu katika sekta hii inaendana na mahitaji halisi ya mchezo huu ambao kwa sasa unaendelea kuchezwa kisasa.

Inafahamika wazi ili kufikia mafanikio ambayo mataifa mengine ya Ulaya yalipo au baadhi ya nchi za Afrika ambazo tayari zimepiga hatua, ni ukweli usiofichika ni lazima TFF kwa kushirikiana na serikali pamoja na wadau kuwekeza kwa makocha pamoja na miundombinu.

Kuwekeza katika makocha, waamuzi na viongozi kutasaidia kufanya kazi za mpira wa mguu kuwa nyepesi kwa sababu kamwe hakutakuwa na sintofahamu ambazo mwisho wa msimu, timu husika huvuna matokeo mabaya na 'zigo' anatupiwa kocha au kiongozi aliyekuwa madarakani. Ni lazima tutumie vyema mafunzo mbalimbali yanayoendeshwa kwa sababu kwa kupata elimu stahiki ya kazi unayofanya, ni wazi mhusika atajiweka sehemu sahihi na kile anachokifanya badala ya kufundisha au kuchezesha mpira kwa kubahatisha.

Tunawakumbusha wale ambao wamesoma kozi hizo, kuyatumia mafunzo yao kwa vitendo na kuacha kuifungia elimu waliyopata kwenye mikoba yao, kwa kufanya hivyo hawatalisaidia taifa kufikia malengo ya nchi kuwa washindani na si washiriki kwenye mashindano mbalimbali ya kimataifa tunayoshiriki.

Endapo wadau wetu watatumia vyema elimu wanazofundishwa na wakufunzi hao kutoka nje, ninaamini hata bajeti ya fedha ya kuhudumia timu za taifa ambayo inatolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan inaonekana imepelekwa eneo sahihi. Zama za kupata mafanikio kwa kutegemea miujiza zimepita, huu ni wakati wa kuona mwanamichezo, klabu au taifa lililowekeza kikamilifu ndilo linafanya vyema kwenye mashindano wanayoshiriki, na ili kufika huko, kila mdau ambaye anashiriki katika mpira wa miguu hapa nchini anatakiwa kuweka weledi katika kila jambo analolifanya.


Mafanikio ya Ujerumani, Brazil au Hispania, yanatokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa kuanzia kwa wazazi, walezi, serikali, makampuni na taasisi zinazofanya kazi kwenye mataifa hayo kwa sababu waliamini uwekezaji wa kweli ndio utawapeleka kwenye ushindi na si vinginevyo.

Unaweza kusema ni jambo dogo kwa wale wasiopenda kuangalia wapi tulikotoka, lakini TFF inatakiwa kupongezwa kwa hatua ambayo Watanzania tumefikia kwa mwamuzi wetu, Frank Komba, kuwa mmoja wa waamuzi wanaochezesha katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), ambazo zinamalizika hapo kesho huko nchini Cameroon. Ukiondoa Komba, huko AFCON yuko Mnyarwanda, Salima Mukansanga, ambaye ameweka rekodi ya kuwa mwanamke wa kwanza kupuliza kipenga kwenye michuano hiyo mikubwa, hali ya kuwa Rwanda haijashiriki fainali hizo kama ilivyo Tanzania.

Kama hili limewezekana kwa kupitia mafunzo mbalimbali yanayotolewa hapa nchini, basi waamuzi, makocha na viongozi wetu huu ni wakati wa kujikita kufanya majukumu yenu kwa weledi, hatimaye jina la Tanzania litang'ara katika michuano ya kimataifa kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Hakuna kisichowezekana, kikubwa ni kila mdau kuitendea vyema nafasi anayoipata na hatimaye nuru njema itaonekana na heshima ya Tanzania itarejea huku neno 'Kichwa cha Mwendawazimu' litabaki historia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Timu ziige Azam kuongeza mikataba wachezaji wake

**KWA** miaka kadhaa sasa huwezi kusikia mgogoro wa mikataba kwa wachezaji wa Azam. Na wala huwezi kusikia mchezaji fulani wa Azam amesajiliwa na klabu nyingine wakati wao wakiwa wanamhitaji.

Pamoja na matatizo mengi iliyonayo Azam kwa kushindwa kupambana na klabu kubwa za Simba na Yanga licha ya kwamba wana pesa na kila kitu, lakini kwa hili la mikataba ya wachezaji wanafaa kupongezwa.

Ukisikia mchezaji wa Azam anakwenda kwenye klabu nyingine, basi ni wao wenyewe hawamhitaji.

Wala huwezi kusikia mchezaji wa Azam ameingia mkataba na klabu nyingine, halafu anaondoka kwa kushindwa kutimiza baadhi ya vipengele vya mkataba.

Kwa Simba na Yanga hili limetokea sana, mfano, Kelvin Yondani kutoka Simba kwenda Yanga, Ramadhani Singano kutoka Simba kwenda Azam, na hata Bernard Morrison kutoka Yanga kwenda Simba.

Kama utakumbuka 2017, ambapo Simba iliwasajili John Bocco, Erasto Nyoni, Shomari Kapombe na Aishi Manula, siyo kwa sababu Wekundu wa Msimbazi walikuwa na ubavu wa kuvunja mikataba, au kugombea mchezaji na timu hiyo, ila uongozi wa Azam wenyewe ulionekana hauwahitaji.

Kulikuwa kama kuna mpango wa kubadilisha mfumo wa klabu kutoka kuwa na wachezaji wakongwe, badala yake kutengeneza wachezaji vijana, mpango ambao nao baadaye ulifeli. Nina uhakika, kama Azam ingekuwa inawahitaji wachezaji hao wabaki wangeweza kufanya hivyo.

Hata marehemu Patrick Mafisango alipotoka Azam kwenda Simba kulikuwa na mabadilishano ya wachezaji, kati ya klabu hizo mbili, mmoja akimchukua mchezaji huyo, huku Azam ikimtwaa, Abdulhalim Humud.

Juzi tu, Salum Aboubakar 'Sure Boy' amekwenda Yanga, na hii ni baada ya wao Azam wenyewe kuonekana wamemchoka.

Lakini kwa sababu Azam haikuhitaji aondoke ilishindikana. Huwa inaziba mianya yote, na hupati hata kipengele kinachoweza kuwabana na kuvunja mkataba mpaka wao waridhie. Hii ndiyo Azam. Huwezi kumchukua mchezaji wao wanayemhitaji kirahisi rahisi.

Hivi majuzi imeingia mkataba wa wachezaji wao chipukizi ambao wamepandishwa Ligi Kuu na wameanza kuwa nyota na kuzungumzwa sana na mashabiki wa soka kutokana na uwezo wao mkubwa.

Wachezaji hao ni Abdallah Kheri 'Sebbo' ambaye ametia kandarasi hadi mwaka 2024, Tepsi Evance na Paschal Mshindo nao wameongezewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja, sasa watamaliza mwaka 2025, badala ya 2024.

Azam kama kawaida yake, huwa ina tabia ya kuongeza mikataba wachezaji wake tegemeo kabla haijamalizika. Wao ukibakisha mwaka mmoja tu, wanakuongeza mwaka mmoja mwingine au miwili. Kama nilivyosema ukiona amebakisha miezi sita yupo Azam, basi huyo hahitajiki na anachotakiwa kufanya ni kutafuta timu nyingine.

Huu ni mfano wa kuigwa na klabu zote nchini ambazo mara nyingi zinasubiri mkataba umalizike na hapo ndipo viongozi wanaanza kukimbizana kukaa na mchezaji kwa ajili ya kusainishana tena.

Na wakati huo zinakuwa zinapata presha kutoka kwa klabu zingine kuwa zinamhitaji, wakati mwingine inakuwa si kweli.

Klabu nyingi za Ligi Kuu, ikiwemo Simba na Yanga zina tabia hiyo. Mfano Simba ililazimika kumsaini Clatous Chama kabla ya kwenda RS Berkane kwa sababu ya presha kuwa anatakiwa na Yanga.

Wakati Azam ikiwaongeza Sebbo, Tepsi na Msindo, Joash Onyango na wachezaji kadhaa wa Simba wanamaliza mikataba yao. Kwa upande wa Yanga Kibwana Shomari, Bakari Mwamnyeto nao wako mwishoni mwa mikataba yao, lakini klabu hizo zimekaa kimya.

Azam yenyewe huwa haitaki maneno, mapema tu, inamaliza shughuli. Ndiyo maana huwezi kusikia wachezaji wake au klabu yenyewe imeingia mgogoro kwenye usajili.

Unapomweka mchezaji wako unayemhitaji mpaka kiasi cha miezi sita, anakuwa na ruhusa ya kuanza mazungumzo na klabu nyingine inaonyesha wazi huna mpango naye.

Tatizo la klabu kubwa za Simba na Yanga, wachezaji wakishasajiliwa na kuwa ndani ya timu huwa hawana thamani. Thamani kwao ni wachezaji wapya, na usajili mpya.

Ndiyo maana unaweza kukuta timu imesajili mchezaji kwa mamilioni ya pesa, lakini imeshindwa kumuongeza mkataba mchezaji wake hadi anamaliza mkataba. Labda awe ni staa kweli kweli kwa kuhofia anaweza kuchukuliwa na timu pinzani. Hongereni Azam, lakini klabu zingine ziondoke huko na si vibaya kuiga Azam FC.

HABARI KITAIFA

# Sabaya akiri kusajili namba kwa kitambulisho chake, kumpa mkewe

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amekiri mahakamani kwamba alitumia kitambulisho chake cha taifa kusajili laini ya simu na kumpatia mke wake, Jesca Thomas.

Sabaya amedai kuwa mchakato wa usajili wa laini za simu upo kwa mujibu wa sheria na si matakwa ya mtu binafsi na kwamba si kosa kwa mujibu wa sheria ya mawasiliano kusajili namba kwa kitambulisho chake na kutumiwa na mtu mwingine.

Sabaya ambaye ni shahidi wa pili kwa mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya uhujumu uchumi na wenzake sita, alikiri jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha.

Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine ni Sylvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Akihojiwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Filex Kwetukia, Sabaya alidai kwamba sheria ya mawasiliano haikusema kwamba ni kosa kusajili laini ya kuazimisha kwa mtu mwingine.

"Katika sheria ya mawasiliano kuna miongozo mbalimbali lakini si kosa mtu kusajili laini kwa kitambulisho chake na kuazimisha kwa mwingine," alidai Sabaya.

Shahidi huyo ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi hiyo, alidai kuwa shahidi wa 13 wa mashtaka, Ramadhani Juma, alipatiwa mkataba wa kununua gari na Jesca Thomas, ambaye mke ni wake.

"Katika utendaji kazi wa Ramadhani hana mamlaka ya kuingilia mahakama kufanya kazi zake," alidai Sabaya na kuongeza kuwa mahakama inaweza kumtia hatiani mtu yeyote hata kama hayupo kwenye hati ya mashtaka.

"Hadi tunavyozungumza, hakuna uthibitisho wowote ambao unathibitisha kwamba namba iliyosajiliwa kwa kitambulisho changu ilikuwa ikitumiwa na mtu mwingine badala ya mimi," alidai.

Pia alidai kwamba shahidi wa 11 wa mashtaka, Hemed Shaban, aliulizwa mahakamani kuwa wakati akikamatwa, aliwakamata na watu wengine wa nne, akiwamo Jesca, na hakukanusha kwamba aliwapeleka katika ofisi za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) makao makuu Upanga, Dar es Salaam.

Kadhalika, alidai kuwa James Wawenje, ambaye ni mfanyakazi wa kampuni ya Vodacom, hakuulizwa wala kuthibitisha kwamba namba yake ya simu ilisajiliwa kwa kitambulisho chake na kutumiwa na mtu mwingine.

Sabaya alidai kwamba video za CCTV hakuziona mahakamani wala hazifahamu zilipokuwa zikionyeshwa wakati Johnson Kisaka, ofisa wa TAKUKURU na Francis Mroso walipokuwa wakitoa ushahidi wao.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Patrobas Katambi, akijibu baadhi ya maswali yaliyoulizwa na wabunge, katika mkutano wa sita, kikao cha nne cha Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Jafo aitwisha zigo bodi mpya ya NEMC

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, ameitwisha majukumu manne Bodi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ikiwamo kuhakikisha mfumo wa vibali vya taka hatarishi unatengenezwa ndani ya siku 45.

Dk. Jafo aliyasema hayo jijini hapa jana alipokuwa akizindua bodi hiyo na kuikabidhi vitendea kazi ili kutekeleza majukumu yake.

"Mfumo wa kielektroniki wa taka hatarishi uje na taarifa sahihi, nitafurahi sana. Hili likiwa ni jambo kubwa ambalo chombo hiki muhimu kitakwenda kulisimamia,"alisema.

Pia aliagiza bodi hiyo kusimamia utekelezaji wa Sera ya Mazingira ya Mwaka 2021, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya serikali.

"Kama mnavyofahamu Sera Mpya ya Mazingira ya mwaka 2021 inategemea kuzinduliwa Februari 12, mwaka huu, sera hii inatoa miongozo ya kisera katika kutatua changamoto mpya za mazingira zinazoikabili nchi yetu,"alisema.

Waziri Jafo alitaja agizo la tatu ni kupitia muundo na majukumu ya NEMC ili kuona kama linatekeleza majukumu yake ipasavyo kwa hali iliyopo sasa kulingana na kero zilizopo katika suala zima la uhifadhi na usimamizi wa mazingira na kutoa ushauri ipasavyo.

Kadhalika, aliwataka kusimamia mapato na matumizi ya fedha na kulisimamia vema Baraza kwa niaba ya Ofisi ya Makamu wa Rais ili miongozo inayotolewa na ofisi itekelezwe kwa weledi.

Alisema ofisi hiyo imejipanga kuchukua hatua mbalimbali zinazolenga kuimarisha masuala ya usimamizi na uhifadhi wa mazingira nchini.

"Tumeshuhudia uhaba wa maji kwenye maeneo yetu na kuwa na mgawo wa maji kupita kiwango hii imetokana na vyanzo vya maji kukauka kutokana na uharibifu wa mazingira, athari za ukame tumezishuhudia baadhi ya maeneo mifugo kufa,"alisema.

Naye Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Prof. Mhandisi Esnath Chaggu, aliahidi kufanyia kazi maelekezo ya Waziri na kuishauri serikali katika masuala muhimu ya hifadhi na usimamizi wa mazingira.

"Wajumbe wa Bodi ni wajibu wetu kufanya kazi kwa bidii na ushirikiano ili tufikie malengo tuliyojiwekea,"alisema.

# Namba za kijeshi taasisi uhifadhi zazinduliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Maliasili na Utalii, imezindua namba za kijeshi zitakazotumika katika magari, mitambo na vyombo vingine vya moto vya Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu Tanzania.

Akizungumza katika uzinduzi huo jijini Dodoma jana, Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Francis Michael, alisema jeshi hilo linafahamika kwa kifupi kama Jeshi la Uhifadhi (JU).

Alisema jeshi hilo linaundwa na taasisi nne za uhifadhi ndani ya Wizara ya Maliasili na Utalii ambazo ni Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanayamapori Tanzania (TAWA) na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

"Sababu kubwa ya kuanzishwa kwa Jeshi la Uhifadhi ni kuimarisha ulinzi wa rasilimali za wanyamapori na misitu na zile zinazoambatana nazo.

"Hii ni kufuatia (kutokana na) kuongezeka kwa ujangili wa wanyamapori wakubwa hususani tembo na faru na kuongezeka kwa uvunaji haramu wa mazao ya misitu katika kipindi cha miaka ya 2000," alisema Dk. Michael.

Pia alisema baada ya uzinduzi wa Jeshi la Uhifadhi mwaka 2018, wizara imekamilisha maandalizi ya nyenzo na vitendea kazi mbalimbali vitakavyosaidia utekelezaji wa mfumo wa kijeshi.

"Baadhi ya vitendea kazi hivyo ni pamoja na kanuni za Jeshi la Uhifadhi, vyuo vya kutolea mafunzo kwa maofisa na askari wake pamoja namba maalumu zitakazokuwa zinatumiwa katika magari, mitambo na vyombo vingine vya moto vinavyomilikiwa na jeshi la uhifadhi" alisema.

Pia alisema pamoja na uzinduzi wa namba hizo, wamepokea magari mapya 15 ya Jeshi la Uhifadhi yatakayotumiwa na TFS.

"Magari haya yamenunuliwa kwa fedha za serikali kama sehemu ya kuimarisha utendaji wa jeshi letu katika kusimamia rasilimali za misitu na nyuki. Magari haya yatagawanywa kwa matumizi katika wilaya za Mlele, Mpanda, Songea, Tunduru, Longido, Rombo, Serengeti, Manyoni, Bahi, Mvomero, Kibaha, Mufindi na Chunya," alisema.

Kamishna wa Uhifadhi wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, alisema kuzinduliwa kwa namba hizo kutasaidia kutambulisha magari pamoja vyombo vingine vya moto vinavyotumiwa na jeshi hilo.

Kuhusu magari hayo 15 yaliyokabidhiwa, alisema yatasaidia kuwezesha shughuli mbalimbali zinazofanywa na jeshi hilo.

Pia alisema magari hayo ni sehemu ya yale 34 ambayo yaliyonunuliwa na serikali mwaka jana na kugharimu takribani Sh. bilioni 5.6.

Kamishna wa Uhifidhi wa TANAPA, William Mwakilema, alisema magari hayo atasaidia kukabilina na ukataji ovyo wa misitu katika hifadhi mbalimbali za taifa.

"Misitu ni uhai hivi sasa katika maeneo mengi nchini misitu imeharibiwa sana magari haya yanakwenda kufanya shughuli ya ulinzi wa misitu pamoja na kukomesha matukio ya ujangiri ili kulinda rasilimali zetu tulizo nazo," alisema.

# Wanafunzi waliopanga uraiani wadaiwa kuishi kama wanandoa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BAADHI ya wanafunzi wa kike ambao wamepanga vyumba kwenye makazi ya watu, maarufu kama gheto, wanaosoma katika Shule ya Sekondari Pandagichiza wilayani Shinyanga, wamedaiwa kusoma huku wakiwa wameolewa kutokana na kukosa usimamizi wa wazazi na walimu.

Shule hiyo, awali ilikuwa na hosteli kwa ajili ya kuhifadhi wanafunzi wa kike, hasa wale ambao wanatoka umbali mrefu ili kuwaepusha na vishawishi njiani vya kurubuniwa na wanaume na kujiingiza katika uhusiano na hatimaye kupata ujauzito au kuolewa na kuacha masomo.

Diwani wa Pandagichiza, Charles Kabogo, alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na Nipashe wakati wa utekelezaji wa mradi wa kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto. Mradi huo unatekelezwa na Chama cha Waandishi wa Habari mkoani Shinyanga, kwa ufadhili wa Mfuko wa Ruzuku wa Wanawake Tanzania (WFT).

Alisema kutokana na ukosefu wa hosteli za wanafunzi wa kike katika shule hiyo, wanafunzi ambao wamepanga vyumba kwenye makazi ya watu, baadhi yao wamekuwa wakijusisha na ngono wengine kusoma wakiwa wameolewa.

"Upangaji huu wa magheto kwa wanafunzi wetu wa kike ambao wanasoma katika Shule ya Sekondari Pandagichiza ni mfumo mbaya sana. Tutazalisha watu malaya na wavuta bangi kwa sababu baadhi ya wanafunzi wanasoma huku wakiwa wameolewa," alisema Kabogo.

"Mikakati ambayo tumejiwekea sisi uongozi wa kata ni kurudisha utaratibu wetu wa wanafunzi kuishi hosteli kama zamani na ni marufuku kwenda kupanga vyumba tena kwenye makazi ya watu. Hata kama wananchi wakinichukia ni sawa. Lazima tuwalinde watoto wetu wasome na kutimiza ndoto zao na si kuishia kuolewa na kuacha masomo," aliongeza.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Shilabela, mahali ambapo wanafunzi wengi wamepanga vyumba, Emmanuel Magadula, alisema tabia za wanafunzi zimekuwa chafu na imefikia hatua wamekuwa wakizurura hadi saa sita usiku.

Baadhi ya wanafunzi wanaosoma shule hiyo ya Sekondari Pandagichiza, walikiri kuwa kutoishi tena hosteli kama zamani na kwenda kupanga vyumba mitaani ni tatizo kwao na kwamba hukumbana na vishawishi hasa pale wanapokosa mahitaji muhimu.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Pandagichiza, George Vangilisasi, alisema hosteli za shule hiyo ziligeuzwa kuwa vyumba vya madarasa lakini baada ya serikali kutoa fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa, hivi sasa kuna ziada ya madarasa manne ambayo yanaweza kutumika kama hosteli.

Alisema mwanafunzi anapokosa usimamizi wa walimu au wazazi na kuishi kwa kujitawala, lazima akumbane na changamoto huko mitaani na ni rahisi kujiingiza kwenye uhusiano wa kimapenzi kutokana na kutokuwako na usimamizi wa walimu na wazazi.



Dk. Erick Mmbando akimpima macho mmoja wa watu waliofika kwenye kliniki ya Kairuki, katika Kituo cha Mabasi cha Magufuli Mbezi Luis, mkoani Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali. Leo wananchi watapimwa magonjwa mbalimbali bure ikiwa ni kuadhimisha miaka 23 ya kifo cha muasisi wa hospitali hiyo, marehemu Prof. Hubert Kairuki **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Kairuki kupima afya bure

**Na Joseph Mwendapole**

KATIKA kuadhimisha miaka 23 ya kumbukizi ya Profesa Hurbert Kairuki, Hospitali ya Kairuki kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hurbert Kairuki (HKMU), imeandaa kambi ya uchunguzi wa afya bure leo ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha kumbukizi ya miaka 23 ya kifo cha mwasisi wa taasisi hizo, Prof. Hurbert Kairuki.

Profesa Kairuki ambaye ni mwanzilishi wa Mtandao wa Afya na Elimu wa Kairuki (KHEN) alizaliwa mwaka 1940 na kufariki dunia Februari 6, 1999.

Huduma hizo za bure kwa siku mbili Jumamosi na Jumapili zitatolewa kama njia ya kukumbuka na kuenzi mchango wake katika sekta ya afya na elimu.

Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Kairuki, Asser Mchomvu, alitaja baadhi ya huduma zitakazotolewa kuwa ni pamoja na uchunguzi wa saratani ya matiti, ushauri na uchunguzi wa saratani ya tezi dume kwa teknolojia ya kisasa na ushauri wa kitaalamu.

Alitaja huduma zingine kuwa ni uchunguzi wa macho (uono) hususani kwa madereva, kupima shinikizo la damu na kisukari, kupima uwiano kati ya urefu na uzito, uchangiaji damu kwa kushirikiana na Mpango wa Damu Salama, chanjo ya UVIKO - 19 kwa wenye uhitaji na uchunguzi wa afya kwa ujumla.

Kuhusu upimaji wa macho, alisema wanawalenga zaidi madereva wa mabasi kwa sababu wanabeba idadi kubwa ya abiria ili kuhakikisha wanakuwa na afya bora ya macho kwa usalama wa abiria.

"Madereva wote waje kupima kwa sababu wanabeba abiria wengi, hivyo lazima afya yao ya macho iwe ya uhakika. Ingawa tutawapima watu wote macho, madereva ndio walengwa zaidi kutokana na kazi yao," alisema.

Mchomvu alisema huduma hizo zitatolewa katika tawi jipya la Kairuki Polyclinic lililoko stendi kuu ya mabasi yaendayo mikoani, maarufu kama Stendi ya Magufuli, Mbezi Luis, kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi mchana.

"Pamoja na huduma hizo, kwa kesho (leo) ambayo ndiyo siku ya kilele, kutakuwa na uzinduzi rasmi wa Kairuki Polyclinic ambapo Kairuki Hospital imesogeza huduma zake kwa wakazi wa Mbezi Luis na viunga vyake," alisema.

Uzinduzi huo, alisema utakwenda sambamba na matembezi ya hiari ya wafanyakazi na wanafunzi wa KHEN yatakayoanzia Goba kwa Robert hadi stendi ya Magufuli.

Wakati huo huo, Mchomvu alisema kati ya Machi na Aprili, kutakuwa na uzinduzi wa kituo cha huduma za uzazi pandikizi kwa wenye changamoto za uzazi (In Vitro-Fertilization - IVF) iliyopo Bunju A Mianzini pamoja na kiwanda cha kutengeneza dawa kilichoko Kibaha Zegereni.

# Kamati ya Bajeti yazuru kwa wanufaika TASAF

**Na Romana Mallya**

KAMATI ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, imewatembelea wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) mkoani Dar es Salaam na kuridhishwa na kazi zinazofanywa na vikundi na kutoa mwaliko kwa vilivyofanya vizuri zaidi kwenda Zanzibar kuwaelimisha wenzao namna wanavyofanya.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Ali Suleiman Amer, alitoa mwaliko huo jana jijini Dar es Salaam baada ya kamati yake kukutana na wanufaika wa TASAF na kujionea namna wanavyopambana kuondokana na umaskini kupitia shughuli mbalimbali wanazofanya za kujiingizia kipato.

Ziara hiyo iliandaliwa na TASAF ambapo msafara ulianzia kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kisha kwenda kwa wanufaika wa mfuko huo wilayani Ilala kwa niaba ya wilaya zingine za mkoa huo.

"Tumejifunza kwa vitendo namna mnavyofanya, ombi langu kwa waratibu wa TASAF Zanzibar, tuwaalike hawa waje kule (Zanzibar) watoe ushuhuda kwa wenzao namna walivyofanikiwa kujikwamua na umaskini, ikiwezekana kikundi chenye mafanikio makubwa kiungane na cha Zanzibar, huo ndiyo Muungano," alisema

Pia aliwataka wanufaika wa mfuko huo ambao wameshapata mafanikio, wajijengee utaratibu wa kuwaachia wengine ili nao wajikwamue na umaskini.

"Tumeona mafanikio yenu, kwa kweli TASAF imewaheshimisha na kudumisha utu wenu, hongereni wanawake, mmeeleza matatizo yenu hapa, tumeyapokea na tutayafikisha sehemu husika," alisema.

Mjumbe wa Kamati hiyo, Mbunge wa Pandani (ACT-Wazalendo), alisema TASAF inaunganisha Tanzania Bara na Zanzibar na kuwaomba wanawake wanufaika kwenda kwao kuwasaidia kwa sababu baadhi ya vikundi huko havifanyi vizuri.

Mnufaika Fatuma Kiswamba aliishukuru TASAF ambayo imempatia elimu ya vikoba ambayo imemwezesha kufanya shughuli za ujasiriamali zinazomsaidia kujenga nyumba ya vyumba viwili na kusomesha watoto.

Mnufaika Mwashabani Dinyango alisema mfuko huo umemwezesha kujenga choo, kuiwekea sakafu nyumba yake na kusomesha watoto.

Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Minazi Mirefu, Kata ya Kiwalani, Oliver Makweta, alisema mtaa wao una jumla ya kaya 1,920. Kati yake, 133 zimo katika utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaosimamiwa na TASAF.

"Desemba mwaka 2019 walipewa mafunzo ya kujiwekea akiba kwa walengwa 150 na watu 119 ndiyo walioitikia wito wa kujiunga kwenye vikundi.

"Walianza kujiwekea akiba kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa chakula katika kaya zao kwa kipindi chote. Wana utaratibu wa kuuziana hisa kwa thamani ya Sh. 1,000 na Sh. 2,000, tuna jumla ya Sh. milioni 22.7 ambazo zimewekezwa na walengwa ni vikundi 10 vya kuweka akiba, mwanachama anaruhusiwa kukopa mara tatu ya hisa zake," alisema.

Alitaja baadhi ya matatizo ni ukosefu wa masoko ya uhakika ya kuuzia bidhaa wanazozalisha, elimu ya ujasiriamali na walengwa wenye umri mkubwa kulalamikia uongozi wa mtaa kutoshiriki kwenye kazi za ajira ya muda ambapo wanazalisha matofali madogo.

Mratibu wa TASAF Mkoa wa Dar es Salaam, Esterine Sephania, alisema awamu ya pili inatekelezwa katika mitaa 304 kati ya 556.

"Mpango wa TASAF 111 kipindi cha pili kwa wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam ambazo ni Ilala, Kinondoni, Kigamboni, Temeke na Ubungo zina kaya zilizolipwa 15,157, zilizoondolewa ni 5,207 na jumla yao ni 20,362," alisema.



HABARI DODOMA

## Serikali yadhamiria kuweka mazingira bora ya uwekezaji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema itaendelea kuboresha na kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji na wafanyabiara ili kukuza uchumi shindani.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, aliyasema hayo jana alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya wizara na taasisi zake kwa wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Viwanda, Biashara na Mazingira, jijini hapa.

Kigahe alisema serikali inaendelea kuweka mazingira bora na kuwalinda wawekezaji na wafanyabiashara ili kukua na kushindana na masoko ya kikanda na kimataifa.

Pia alisema kuwawezesha kuanzisha viwanda vidogo vidogo vitakavyosaidia nchi kujitosheleza kwa bidhaa muhimu mbalimbali ikiwamo sukari.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, David Mwakiposa, alitaka wizara kuendelea kuboresha na kuweka mazingira bora na wezeshi kwa wawekezaji na wafanyabiashara, kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma hadi vijijini.

Pia alisema kusimamia uzalishaji wa bidhaa mbalimbali nchini kwa kutumia malighafi za ndani ili kukuza uchumi wa nchi.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Erick Shigongo, aliishauri wizara kuanzisha mfuko wa ubunifu nchini (Tanzania Innovation Fund) kwa lengo la kulea, kuendeleza na kukuza vijana wabunifu wa bidhaa mbalimbali ambazo zinaweza kuanzisha viwanda vikubwa vya uzalishaji vitakavyoongeza pato la taifa na ajira.

Baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo walitoa maoni na mapendekezo mbalimbali yanayolenga kuboresha utekelezaji wa jitahada mbalimbali katika kuendeleza sekta za uwekezaji, viwanda na biashara.

Walishauri kuboreshwa kwa mifuko ya kuwezesha wajasiriamali, kulinda wazalishaji wa ndani, kutafuta masoko ya uhakika ya mazao nje ya nchi, kutoa elimu kwa umma na kuongeza ubunifu katika kitumia malighafi zinazopatikana nchini katika kutengeneza bidhaa mbalimbali.

Awali, akitoa taarifa hiyo ya utekelezaji wa bajeti ya wizara, Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Alfred Mapunda, alisema katika utekelezaji wa bajeti hiyo, wizara imepata mafanikio mengi ikiwamo uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara.

Pia alisema uanzishaji wa kongani za viwanda, uboreshaji wa masoko ya mipakani, utoaji wa huduma kwa njia ya mtandao na kuimarisha uhusiano wa kibiashara baina ya nchi, kikanda na kimataifa.

# Aliyedai kudhulumiwa abainika kuwa amemdanganya Rais Samia

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma limebaini Veronica Alex amemdanganya Rais Samia Suluhu Hassan kuwa amedhulumiwa mali zake wakati alishindwa kesi mahakamani.

Februari 2, mwaka huu, mwananchi huyo alipaza sauti ya kudhulumiwa katika kilele cha Siku ya Sheria wakati Rais Samia alipokuwa akihutubia, hali iliyomlazimu kuelekeza wasaidizi wake kumsikiliza.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Onesmo Lyanga, alisema wamebaini pia Veronica si mtumishi wa umma kama alivyodai.

"Nawaomba wananchi msipende kukimbilia juu juu. Suala liko wazi, mahakama zipo na jeshi lipo. Msipende kuwadanganya viongozi,"alisema.

Kamanda Lyanga aliwataka wananchi kwenda kutafuta haki mahakamani na si kukimbilia katika hafla na kutaka kuwavamia viongozi ilhali si haki kisheria.

Alisema wamemuonya Veronika na wananchi wengine wenye tabia hiyo kwa kuwa wanatenda kosa.

Lyanga alisema hatua kali zitachukuliwa kwa yeyote atakayeidanganya Mahakama na Jeshi la Polisi na kukimbia kwa Rais kutaka msaada.

"Bado milango iko wazi kwa Veronica kwenda kukata rufani ili kusikilizwa shauri lake na kupata haki yake," alisema.

Kamanda Lyanga alisema jeshi hilo liko tayari kuwasikiliza wananchi wanaofika kwa ajili ya kutafuta haki zao za msingi pale wanapodhulumiwa.



Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde (kushoto), Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (wa pili kushoto), Naibu Meya wa Jiji la Dodoma, Emmanuel Chibago (wa pili kulia) na Mkurugenzi wa Jiji, Joseph Mafuru, wakijaribu kuendesha pikipiki zilizotolewa na Jiji hilo, kwa ajili ya kuwakopesha vijana, jijini humo juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Ummy ataka fedha mradi kujenga miundombinu afya mama na mtoto

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ameagiza fedha za mradi wa kuwekeza kwa watu ziboreshe huduma za afya kwa kujenga miundombinu ya kutolea huduma kwa wajawazito, mama na watoto na kununua vifaa tiba.

Mradi huo unatekelezwa kwa kushirikiana na Benki ya Dunia ambao una thamani ya zaidi ya Dola za Marekani milioni 200, unalenga kuboresha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto nchini.

Ummy aliyasema hayo jana alipokutana na kufanya mazungumzo na Mwakilishi Mkazi wa Benki ya Dunia nchini, Mara Warwick, katika ofisi za wizara jijini hapa na kuishukuru benki hiyo kwa kuendelea kuwa mshirika wa karibu wa maendeleo kwa Tanzania na kusaidia sekta ya afya nchini.

"Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inatekeleza mradi wa 'Investing in People' (Kuwekeza kwa Watu). Fedha hizi zielekezwe kwenye kuboresha huduma za afya kwa kujenga miundombinu ya kutolea huduma kwa wajawazito, mama na watoto, kujenga wodi za watoto wachanga pamoja na kununua vifaa tiba," alisema.

Kuhusu mapambano dhidi ya UVIKO-19, Waziri Ummy alisema serikali kupitia Wizara ya Afya inaendelea kutoa chanjo nchini kote na kuikaribisha benki hiyo kushirikiana na serikali katika mapambano hayo.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, aliomba benki hiyo kushirikiana na serikali kuvutia wawekezaji wa viwanda vya dawa na chanjo nchini.

Warwick alipongeza juhudi zinazoendelea kutekelezwa na serikali na kuahidi kuendelea kushirikiana ili kuboresha huduma za afya nchini pamoja na mapambano dhidi ya UVIKO-19.





# SMZ yapata dawa kukatika umeme

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini imesema kujengwa kwa mnara ambao unatumia nishati ya umeme wa jua utapunguza kukatika kwa umeme mara kwa mara.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk Mngereza Mzee Miraji, alisema hayo jana wakati akifungua mkutano wa wadau wa nishati na madini katika ukumbi wa Hoteli ya GoldenTulip, Zanzibar.

Alisema mradi huo utaleta mabadiliko zaidi ya kasi ya uchumi hasa kwa upande wa sekta ya uwekezaji Zanzibar.

Pia alisema mradi huo wenye thamani ya zaidi ya Dola milioni 140 za Marekani, utalenga katika maeneo ya mikoa ya Kaskazini na Kusini Unguja.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Maji, Nishati na Madini imejipanga kutekeleza kwa malengo yaliyokusudiwa.

Akiwasilisha mada, Sayyid Omar Abdullah Idarous kutoka Idara ya Nishati na Madini, alisema kukamilika kwa mradi huo itakuwa dawa ya kukatika katika kwa umeme Zanzibar na kutatoa nafasi ya upatikanaji wa umeme wa uhakika.

Pia alisema mradi huo utapunguza uharibifu wa mazingira pamoja utunzaji rasmi na kupunguza gharama za matumizi yasiyo ya lazima.

Alisema mradi huo utatengeneza miundombinu imara ya njia za umeme na kuondoa uharibifu wa njia hizo.

Hata hivyo, alisema mradi huo unalenga zaidi vijijini kwa vile imeonekana kuwa maeneo hayo upatikanaji wake wa umeme ni mdogo.

Naye Mratibu wa Mradi, Saleh Said Suleiman, alisema mradi huo ni wa 600 na utatekelezwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) na Wizara ya Nishati na Madini. Alisema utakuwa unafanya kazi zaidi katika kisiwa cha Unguja kwa vile ndiko unakojengwa.

Aidha, alisema sababu ya kujenga mnara huo ni kufanywa kwa tathmini kuwa hali ya upatikanaji wa umeme ni changamoto katika vijiji hivyo.

Mradi huo, alisema unatekelezwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia na umebarikiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na umeshazinduliwa na tayari uko katika utekelezaji.

Alisema mradi huo unafanya kazi siku zote na utakuwa unafanya kazi kwa vile umejengewa vifaa vya kuhifadhi mionzi na zaidi ya watu 300,000 watanufaika nao.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza wakati akifungua mafunzo ya upangaji wa vipaumbele na uaandaaji wa mipango ya maendeleo yaliyoandaliwa na Taasisi ya Tony Blair pamoja na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), katika Ukumbi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) Kampasi ya Maruhubi, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Bima ya afya yaanzishwa rasmi Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar imesema imeamua kuanzisha huduma ya bima ya afya ili kuwasaidia wananchi wake wote kupata huduma bora za afya.

Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, alisema hayo jana wakati akifungua warsha ya uanzishaji wa mfuko wa bima ya afya kwa wananchi wa Zanzibar. Hafla hiyo ilifanyika katika ukumbi wa Shirika la Bima, Mipirani, mjini Unguja.

Alisema hatua hiyo itawasaidia wananchi kupata huduma hiyo kwa ufanisi pindi watakapoitumia ipasavyo.

Waziri Mazrui alisema huduma hiyo itasaidia kufanikisha malengo ya serikali ya kuwaletea maendeleo bora wananchi wake kupitia sekta mbalimbali ikiwamo afya.

Alisema nchi nyingi hivi sasa wananchi wake wamekuwa wakitumia huduma hiyo, hivyo imefika wakati Zanzibar nayo kuelekea katika utaratibu huo ili kuwasaidia wananchi kupata huduma katika misingi imara na iliyo bora.

Kutokana na mpango huo, aliwasisitiza watendaji watakaohusika na kitengo hicho, kuhakikisha wanafanya kazi kwa weledi na kutoa elimu zaidi kwa wananchi ili kufahamu malengo ya serikali katika kuanzisha bima hiyo na kupata uelewa juu ya umuhimu wa kutumia huduma hiyo.

Alisema serikali itahakikisha inazidi kuimarisha mifumo ya utoaji wa huduma za afya ikiwamo miundombinu, majengo, dawa na wataalamu wa kutosha ili mpango huo utapoanza, ufanye kazi kwa kwa ufanisi na kuleta tija kwa wananchi wote.

Mratibu wa Uanzishaji wa Mfuko wa Bima ya Afya Zanzibar, Yassin Ameir Juma, alisema kwa hatua ya mwanzo watahakikisha kila mwananchi anatambua uwapo wa bima ya afya na kupata fursa ya kujiunga na mfuko huo.

Alisema atahakikisha mfumo huo unakuwa na teknolojia bora ambao itawatambua wanachama wa mfuko kwa mujibu wa hali zao kimaisha.

# Maambukizi VVU wajawazito chini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mtendaji wa Tume ya Ukimwi Zanzibar (ZAC), Dk. Ahmed Mohammed Khatib, amesema bado maambukizi ya virusi vya ukimwi (VVU) kwa wajawazito Zanzibar yako chini ya asilimia moja.

Kutokana na mafanikio hayo, alisema ni wajibu wa wananchi kuhakikisha wanapima afya zao ili kupunguza maambukizo mapya ya VVU na kuwakinga watoto kuwa na maambukizi.

Alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo kwa waandishi wa habari Zanzibar kuhusu Ukimwi katika ukumbi wa Malaria, Mwanakwerekwe.

Dk. Khatib alisema huduma za kuzuia maambukizi kutoka kwa mjamzito anayeishi na VVU kwenda kwa mtoto zinaendelea kutolewa ikiwemo dawa za kupunguza makali ya virusi hivyo (ARV).

Alisema hatua hiyo imekuwa na mafanikio makubwa katika kukabiliana na maradhi hayo na mama wengi kuendelea kuzaa watoto wakiwa salama.

Alisema ikiwa mama atakuwa na maambukizi, anapewa dawa hizo ili kumzaa mtoto wake na kuwa salama.

Dk. Khatib alisema kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2021, wajawazito 48,860 Unguja na Pemba walipimwa afya zao na 111 waligundulika kuwa na maambukizi mapya ya VVU.


Pia alisema watoto waliozaliwa na mama wenye maambukizi ya VVU, waliofanyiwa uchunguzi walikuwa 304 na watoto nane waligundulika kuwa na VVU.

Alisema lengo la nchi ni kumaliza maambukizo kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na ifikapo mwaka 2025 hakuna mtoto anaezaliwa na VVU.

Mkurugenzi huyo aliisisitiza jamii kuacha unyanyapaa kwa watu hao na kuwaunga mkono ili kumaliza kabisa maambukizo mapya ya VVU.

Meneja Mradi wa Afya Kamilifu Zanzibar, Dk. Mohammed Hassan, alisema wanashirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Afya na Tume ya Ukimwi, taasisi zisizo za kiserikali na viongozi wa dini wanakuwa na lengo la kupambana na VVU na Ukimwi hasa katika upimaji na kufikia asilimia 95

Aliwasisitiza wanahabari kufikisha ujumbe kwa jamii kuhusu VVU na Ukimwi na kuwasisitiza wananchi kukubali mikakati iliyowekwa katika kupambana na ugonjwa huo.



# JUA LINAZAMA Diamond atahadharishwa mapema

MWEZI Desemba mwanamuziki nyota nchini, Diamond Platnumz, aliachia ngoma yake mpya inayoitwa 'Unachezaje' , ambayo iliibua maneno mengi kutoka kwa mashabiki wake.

Wimbo huo ambao ulifanyiwa promo kubwa, haukuweza kukidhi kiu ya mashabiki, huku msanii huyo akilaumiwa kuwa alitoa ngoma ambayo hailingani na kipaji chake.

Hata hivyo, wapinzani wake kama Harmonize na Ali Kiba, wanatabasamu wakisubiri kuona msanii huyo akiteleza ili na wao waweze kutawala soko.

Hivi karibuni Dimond ameonekana akiwa nje ya nchi akiandaa kazi zake, hata hivyo baadhi ya watu wake wa karibu wanasema yuko katika harakati za kuandaa Albam yake mpya ambayo itawashirikisha wanamuziki wengi wa nje.

Wachambuzi katika masuala ya muziki wanasema, kinachoendelea sasa kwa msanii huyo ni jitihada zake za kubaki katika chati, lakini dalili zinaonekana anaweza kuteleza na kushuka kwa kasi.

Shukuru Akida, amesema kuwa sanaa ya muziki wa kizazi kipya sawa na mchezo wa soka, kwani umri ukisonga mbele na kujiamini kupita kiasi kunaweza kumshusha msanii haraka na asiweze kurudi tena.

"Wapo wasanii wa kizazi kipya ambao kwa sasa hawapo tena kutokana na umri wao kuwa mkubwa wameshindwa kufikiria mahitaji ya soko, pamoja na kujiamini kupita kiasi , kiasi ambacho waliona wao ndio kila kitu," amesema.

Amesema Diamond na timu yake isipokaa na kuangalia kwa umakini wanaweza kupotea njia baada ya kuamini kila wanachokifanya wanaweza kufanikiwa.

Ameeleza kama mwanamuziki huyo anajiandaa kuachilia Albam, basi anatakiwa kuhakikisha nyimbo zake zinakuwa tofauti na zile za mwanzo ili kuonekana ana kitu kipya.

"Mashabiki wa muziki hawataki kusikia kitu kilekile, nawashauri ni wakati wa kutoa nyimbo nzuri na tofauti na zile za awali kwani wameona mapokeo ya wimbo wa Unachezaje ulivyokuwa," ameongeza kusema.

BASI SAWA

## Country Boy anapenda mwendo kasi



Msanii wa Hip hop Bongo, Ibrahimu Madingo, maarufu kama Country Boy amefunguka kuwa mziki wake unahitaji kasi kubwa ili kufikia malengo yake kwa haraka.

Country Boy ambaye ametoka katika lebo ya Konde Gang hivi karibu, amesema msanii akiwa kwenye kundi au lebo lazima uende nao sawa, hivyo yeye pia anapenda kwenda kasi.

"Mziki wangu nahitaji uende kasi, mkiwa kama kundi lazima mwende sawa ili usionekane tofauti na wengine " Amesema Country Boy.

Amesema mziki wa hip hop unahitaji uwe bize kila wakati hasa katika maonyesho na matukio mbalimbali yakuimba.

## YJ afanya kufuru mbele ya Salt Bae'



MKALI wa Bongo Fleva, Yakuti Joseph a.k.a YJ, ameonyesha jeuri ya fedha baada ya kuonekana akila bata katika mgahawa unaohudumia mastaa wakubwa duniani wa Nusri Et, ambao upo chini ya mchoma nyama maarufu Salt Bae.

Salt Bae ambaye anamiliki mgahawa huo uliopo Dubai, amewahi kuwahudumia mastaa wakubwa kama vile Lionel Mess, Cristiano Ronaldo, Paul Pogba, DJ Khaled, Maradona, Drake na hapa Bongo ni Ben Pol.

Amejizolea umaarufu mkubwa kwa mtindo wake wa kuhudumia wateja na kunyunyiza chumvi kwenye nyama.

YJ ameliambia BT kuwa yupo Dubai kwenye mapumziko na biashara zingine huku akiendelea kuandaa ngoma mpya kwaajili ya mashabiki zake baada ya 'Chambwembwe' kufanya vizuri.



## Zuchu azidi kuruka kivuli chake

Msanii wa Bongo Fleva kutoka katika lebo ya WCB, Zuhura Omary Othumani, maarufu kama Zuchu, anaendelea kukana kuwa na uhusiano wa kimapenzi na bosi wake Diamond Platnumz.

Akizungumza wiki hii katika mahojiano na Wasafi Fm, amesema kuwa yeye na bosi wake huyo hawapo katika uhusiano wa kimapenzi kama watu wanavyotafsiri. Amesema huenda maneno au uvumi huo unatokana na ukaribu walionao wa kikazi na mara nyingi wamekuwa pamoja kwa ajili ya kupewa maelekezo ya kazi ya mziki na si vingine.

"Mimi na Bosi wangu hatupo kwenye mahusiano kama watu wanavyotafsiri yeye ni bosi ataendelea kuwa bosi" amesema



## Ferdinard BF sasa mwendo 'Shikilia' usianguke

MWANAMUZIKI mwenye asili ya Kongo anayeishi Texas, Marekani, Ferdinard BF, amewaomba mashabiki wa muziki Bongo kuipokea video yake mpya ya wimbo 'Shikilia'.

Akizungumza na BT jana, Ferdinard, amesema ndani ya wimbo Shikilia ametumia mtindo mpya kabisa wa muziki wenye ladha tofauti na nyimbo nyingi za Waafrika.

"Najitahidi kutumia ubunifu wangu kufanya muziki ambao utabeba asili ya Afrika, naomba wapenzi wa muziki mzuri kuutafuta wimbo wangu Shikilia ambao upo kwenye chaneli ya YouTube ili waonje ladha hii mpya ya muziki," amesema Ferdinard.

## HAPA WANAUME WAMEPIGWA

**Na Adam Fungamwango**

WIKI iliyopita tuliona nyimbo za muziki wa dansi ambazo wanaume 'wamewapiga kamba ' sana wanawake. Wamewadanganya wakadanganyika. Nyimbo tulizoziweka hapa ni 'Karubandika' na 'Mayanga' zote za wa Maquiz Original, 'Pendo' wa Bima Lee, 'Homa Imenizidia' wa Orchestra Safari Sound ya mtindo wa Ndekule, na 'Karumanzira' wa Juwata Jazz msondo Ngoma.

Zote hizi ni mwanaume wakiwadanganya wanawake, wengine wakiwatoa vijijini na kuwaleta mjini wakidai ni maofisa, wengine wakitaka waachike kwa waume zao ili wawaoe. Wenyewe wanasema eti tangu enzi za mababu mwanaume akimpenda mwanamke, uongo lazima usemwe japo kidogo.

Lakini si wanaume tu. Hata wanawake nao wapo wadanganyifu. Wiki iliyopita tuliona wanaume wakiwapiga 'kamba' wanawake. Leo sasa wanaume wanapigwa na wao.

**MILIMA YA KWETU-SUPER RAINBOW**

Wimbo huu ni wa mwanzoni mwa miaka ya 1980, ulitungwa na marehemu Eddy Sheggy akiwa na Super Rainbow. Unamzungumzia mwanaume anayelalamika kumtoa mwanamke kijiji na kumleta mjini. Bibie akabadilika, kila kitu kakijua. Akageuka yeye ndiyo mtoto wa mjini. Akaanza kumfanyia vituko mumewe, huku akimletea mabwana hadi mlangoni. Mwishowe akamkimbia kabisa.

Bwana anarudi kwao Tanga yupo ndani ya basi anawaza akirudi atasema nini, maana alimuoa kwa harusi ya kifahari, walitoka wawili, leo anarudi peke yake.

**SOLEMBA-JUWATA JAZZ BAND**

Katikati ya miaka ya 1980, marehemu Nico Zengekala akiwa na Juwata Jazz Banda alitunga wimbo wa 'Solemba' Maudhui yake ni jamaa aliyelalamika kuwa aliahidiwa na mwanamke mmoja aende nyumbani kwake baada ya kuelewana kimapenzi. Lakini alichokikuta huko ni simulizi.

Yalikuwa ni matusi na dharau, na demu akadai kuwa hamfahamu huyo kijana, badala yake anamsumbua bure, hana mpango naye. Bwana limemshuka.



**SHAHADA WA UVUMILIVU-DDC MLIMANI PARK**

Ni kisa cha kusikitisha, cha jamaa mmoja aliyechukuliwa mke na jamaa mmoja ambaye alimuahidi kumjengea nyumba. Mke akamkimbia kwenda kwa huyo hasidi. Sasa katika wimbo huu rafiki zake wanamwita aende Sikinde Ngoma ya Ukae wakamtunukie shahada ya uvumilivu, kwani pamoja na maumivu, lakini hakutaka kulipiza kisasi.

**NIMEACHWA KWENYE MATAA-WASHIRIKA BAND**

Ni utunzi wake Eddy Sheggy, mwishoni mwa miaka ya 1980, alitunga kibao hiki, cha jamaa aliyedanganywa na mpenzi wake anakwenda kumsindikiza mjomba wake Uwanja wa Ndege anasafiri, akaenda naye. Kufika huko, kumbe ni mpenzi wake na tiketi amekatiwa. Yeye akaachwa hapo, mpenzi wake na jamaa wakaingia ndani ya ndege.

**FARIDA-TABORA JAZZ BAND**

Wimbo huu ulifyatuliwa kwenye miaka ya 1970 na bendi ya Tabora Jazz Band. Kisa hiki ni cha jamaa aliyemchukua Farida Mwanza na kumleta mjini Dar. Alipokwenda safarini Tanga, aliporudi hakumkuta mwanamke huyo. Alimtoroka na kila kitu kamchukulia. Hapa mwanaume kapigwa.

## Ndele Binti Mrembo: Hapa ni nasa udate

**Na Adam Fungamwango**

ZAMANI, miaka ya 1980, bendi ya Super Matimila ilifyatua wimbo mmoja unaitwa 'Kivunja Undugu'. Maudhui ya wimbo huu yametaja kati ya pesa, mali na mwanamke, chochote kitakachovunja undugu hapo ni mwanamke na si vinginevyo.

Wakasema ndugu yako anaweza kuiba pesa, au gari unaweza kumsamehe, lakini si kukuchukulia mke. Hilo ni jambo lingine kabisa. Hili ndilo linaloonekana kwenye filamu ya 'Ndele Binti Mrembo'. Ni kisa kinachoonyesha kuwa siku zote urembo ni ulimbo.

Imechezwa na Mohamed Fungafunga, maarufu kama mzee Jangua (sasa marehemu), Haji Adam Mariam Omari, Ismail Mahundi na wengineo.

Inaanza kuonyesha chifu wa himaya ya Linole analetewa mwanamke mmoja aitwaye Ndele mbele yake. Walinzi wanamwambia kuwa mwanamke huyo amemuua mumewe Adili kwa sababu amemkuta akiwa kwenye mwili wa marehemu mumewe shambani, akiwa ameuawa .

Sheria zinasema kuwa kwa mwanaume akifanya kosa hilo atafukiwa mzima mzima ardhini akiwa hai, lakini mwanamke, ananing'inizwa juu ya kamba akinyimwa chakula na maji hadi afe.

Ndiyo adhabu anayoipata Ndele kwa chifu mzee Jengua. Usiku rafiki yake anampelekea maji na chakula porini, mazungumzo yao, yanasikika na baadhi ya walinzi wa Chifu.




Wanapelekea habari kuwa huenda Ndele si muuaji halisi. Chifu anaamuru aletwe, anaulizwa hajibu kitu. Lakini baada ya kubanwa akataja muuaji ni kiatu.

Ukweli hamjui muuaji, ila alipokwenda shambani na kumkuta mumewe ameuawa, alikiona kiatu cha mtu ambaye hakitambui.

Chifu anaamuru walinzi wamtafute mwenye kiatu hicho. Wanapita kote. Wanafika nyumbani kwa mdogo wa marehemu Twaha. Mtoto wake anakiona kiatu hicho anasema ni cha baba yake. Kingine kiko wapi? Shaaban anasema aliona siku moja baadaye anakifukia. Anapeleka walinzi sehemu hiyo, wanafukua, siyo tu wanakuta kiatu kimoja kilichobaki, bali hata nguo zilizokuwa na damu.

Zinapelekwa kwa chifu na muuaji halisi akawa amepatikana na kukamatwa. Anaulizwa kwa nini alimuua ndugu yake? Kumbe naye pia alimpenda Ndele. Alikuwa na wivu kwa kaka yake juu ya mwanamke huyo. Awali yeye alimhitaji, lakini baadaye akampenda kaka yake.

Kuna siku akambaka. Mke alifanya siri, lakini mumewe alikuja kusikia, na ndipo ugomvi mkubwa ukazuka, na mdogo kumuua kaka yake. Twaha akahukumiwa adhabu ya kufukiwa mzima ardhini.



## Simon Cowell avunjika kiganja

JAJI maarufu wa shindano la kuibua vipaji la America Go Talent' Simon Cowell, amevunjika kiganja cha mkono baada ya kupata ajali ya baiskeli.

Ajali hiyo ilitokea wiki iliyopita karibu na nyumbani kwake eneo la West London, nchini Uingereza.

Kulingana na mtandao wa PageSix, jaji huyo ambaye anapendwa zaidi, alianguka chini baada ya baiskeli kuteleza, lakini hali yake inazidi kuimarika.

Gazeti la The Sun liliripoti kuwa Cowell ilikuwa bahati kuwa hai kutokana na mwendo wa kasi aliokuwa akiendesha baiskeli yake.



## Rihanna umewaziba midomo

MWANAMUZIKI wa Marekani mwenye asili ya visiwa vya Barbados, Rihanna amepongezwa kwa hatua yake ya kuamua kubeba ujauzito wake wa kwanza.

Imeelezwa Rihanna anatarajia kupata mtoto huyo ambaye baba yake ni rapa maarufu nchini humo, A$AP Rocky.

Rihanna anajulikana kwa tabia yake ya kubadilisha wanaume na kula maisha kiasi ambacho hadi anafikia umri wa miaka 31, hana mtoto.

Baadhi ya mastaa wamejitokeza kumpongeza kwa hatua hiyo na kumtaka kumuomba Mungu ajifungue salama na kumpata mtoto wake wa kwanza.


## Kanye uliona wa nini, wenzio ni dhahabu

SASA ni vita kamili! Imeelezwa rapa wa Marekani, Kanye West, anatuhumiwa kueneza uvumi kuwa Pete Davidson ambaye ni mpenzi wa Kim Kardashian kuwa anashiriki mapenzi ya jinsia moja na pia ameathirika na Ukimwi.

Davidson kwa sasa amemchumbia aliyekuwa mke wake Kim na kwamba imeelezwa kitendo hicho kimemkwaza Kanye kupita kiasi.

Kulingana na PageSix, rapper huyo bilionea ameanzisha ugomvi huo kwa kuwaambia watu mbalimbali waliokuwa karibu naye kuwa Davidson ni mtukutu pamoja na kutishia kuwa atampiga nyota huyo wa wimbo wa "Saturday Night Live".





## Chris subiri dunia ikufunze

MWANAMUZIKI nyota wa Marekani, Chris Brown, anakabiliwa na tuhuma ya ubakaji na inaweza kumgharimu kiasi cha dola milioni 20 kama fidia.

Kulingana na TMZ, Brown anatuhumiwa kumfanyia kitendo hicho dansa na mwanamuziki anayefahamika kama Jane Doe.


Katika madai hayo, inaelezwa Brown, alimwalika Doe katika jumba la kifahari linalomilikiwa na P Diddy katika kisiwa cha Star na ndipo alipofanikiwa kufanya unyanyasaji huo.

## Adele tulia, Paul atabaki wako tu

MWANAMUZIKI kutoka Uingereza, Adele , amewakejeli wale ambao wamekuwa wakidhani kuwa uhusiano wake na Rich Paul umevunjika.

Nyota huyo wa muziki kupitia ukurasa wake wa Twitter, ameandika ujumbe ambao amewalenga watu wanaoeneza uvumi kwamba yeye na Paul wana tofauti.

"Nina furaha sana kusema kwamba ninatumbuiza huko Brits wiki ijayo, pia nitajitokeza kumuona Graham kwa mazungumzo kwenye kochi, na Rich anatuma ujumbe wa mapenzi," alitwiti.



# CCM INAPOTIMIZA MIAKA 45

## ●Utii wa kisiasa utamwezesha Samia kufanya mageuzi
## ●Ufafanuzi kiitikadi utapunguza misuguano CCM



**Na Ani Jozeni**

UKIANGALIA mabadiliko nchini kuanzia kipindi cha awamu ya kwanza, yaani miaka 60 tangu uhuru upatikane, moja ya masuala yanayojitokeza ni jinsi serikali awamu tofauti zimefaulu kuleta mabadiliko ya kina katika sera, na kuungwa mkono ndani ya chama tawala.

Licha ya kuwa serikali zote zilifaulu kupata uungwaji mkono uliohitajika, kulikuwa na viwango tofauti vya misuguano katika chama tawala, hali inayoendana kwa kiasi fulani na hisia za makundi tofauti katika jamii.

Suala hapa ni kama mageuzi yote yanawezekana uongozi ukitaka, au iko mipaka ya wazi?.

Kimsingi, kila kiongozi aliyeko madarakani au kila serikali inayosimamia shughuli za nchi inakuwa huru kufanya mageuzi inayotaka, au inayoona yanafaa.

Chama tawala uongozi wake na ngazi tofauti za wanachama wana kazi moja tu, nayo ni kusaidia kufikia malengo tarajiwa. Ila hali inapoanza kuvurugika inabidi juhudi zifanyike kuwaweka watu pamoja ili kusitokee migawanyiko.

Kila kipindi cha uongozi kina migawanyiko yake, ambayo inaendana na kiwango cha kukubalika kwa uongozi katika jamii pana. Watu wanawasilikiza viongozi waliochaguliwa, ila kimsingi kila raia humsikiliza kiongozi mkuu kwa wakati wake mwenyewe, kama anavyopiga kura.

Kuelekea mwisho wa mwaka jana, taasisi ya utafiti uchumi ya REPOA ilifanya kongamano kwa kushirikiana na ubalozi wa Marekani, wataalamu waliokusanyika walijadili mitazamo ya kitaifa kuhusu njia zinazofaa kuleta maendeleo, mabadiliko yake katika kipindi cha miaka 6 na miaka 45 ya CCM, mada ya msingi ikitolewa na mwenyekiti wa bodi ya REPOA, Profesa Rwekaza Mukandala.

Anayeelewa utafiti katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam anaweza akapata picha ya majadiliano, yaani ladha za mipango ya miaka mitano, sera za Ujamaa, mageuzi, ulipaji madeni, ubinafsishaji na uwekezaji.

Jambo ambalo mchambuzi kutoka nje asingetazamia kuwa litajadiliwa katika kongamano kama hilo ni kama kuna tatizo la msingi katika sera za uchumi tangu uhuru, na serikali zilizotangulia zilifanya nini kukabiliana nalo, na zilifikia wapi.

Ni kwa hali hiyo tu ambako sera za awamu ya sita angalau hadi tulipofikia zinaweza kuangaliwa, siyo kama mwendelezo tu au kutatua matatizo ya serikali zilizotangulia, ila uwezo wa kukabiliana na tatizo la msingi linaloibakiza nchi katika umaskini.

UDSM kwa suala hilo haina tofauti na mwelekeo serikalini, kuwa tumepiga hatua, kazi inaendelea.

Awamu ya sita kuna utofauti na awamu tatu na hata nne zilizopita, hatua zinazochukuliwa sasa zinaonyesha mwelekeo thabiti wa taswira ya taifa.

Ni kipindi kinachoendana na kuingizwa kwa mfumo wa vyama vingi ambako wengi katika CCM hawakufurahia kwani walihofia umoja wa nchi unaweza kuvurugwa kama upinzani ukiruhusiwa.

Suala la msingi ni mabadiliko ya sera za uchumi unaofanywa na awamu ya sita ni sawa na ile awamu ya pili.

Serikali ya awamu ya pili iliungwa mkono kwa miaka saba ya kwanza, yaani kipindi chote cha muhula wa kwanza wa Rais Ali Hassan Mwinyi na kipande kidogo tu cha muhula wa pili, alipongia madarakani kulikuwa na uhaba wa takriban kila kitu, wajasiriamali wakijitahidi kutengeneza sabuni, kalamu, kupitisha bidhaa mipakani na hasa upande wa Kenya, n.k. Alichokifanya Rais Mwinyi ni kufungua milango ya kuingiza bidhaa, hivyo wafanyabiashara wa ndani na ndugu zao walioko nje wakapata nafasi ya kuingia sokoni, kuleta bidhaa za kila aina.

Mabadiliko hayo yalibadilisha ladha ya maisha ya kila siku, ikawa hakuna tena tatizo la uwepo wa vitu ila uwezo wa kuvipata inategemea kila mtu na 'mipango' yake. Hatua hiyo iliendana na jitihada za kubadili Miiko ya Uongozi ili wana-CCM waweze kuwa wafanya biashara au wakulima wa kisasa wa kuajiri wengine, au wachukue mikopo wajenge nyumba za kupangisha.

Ni wakati huo ambako CCM kimsingi iliacha itikadi ya kimapinduzi, na minong'ono iliendelea chini kwa chini.

Kilichomsaidia Rais Mwinyi na kitamsaidia pia Rais Samia ni kuwa mabadiliko hayo yaliwasaidia wengi na hivyo yalipendwa kote nchini, na hata ndani ya CCM hoja za kiitikadi zilipungua nguvu wakati wajanja wanaanza kutengeneza pesa.

Tatizo likawa serikalini kwa mashirika ya umma, kuwa nao pia wawe na mazingira ya kupata fedha watakavyo, ili waendelee katika nafasi za juu kijamii ambazo zilikuwa sasa zinaenda kwa wanaofanya biashara.

Ukashamiri msuguano ulioanza mwaka 1982 wa mashirika ya umma kuwa huru, yasiingiliwe na mawaziri yaani wanasiasa.

Mabadiliko ya awamu ya tano yalikuwa ni mapinduzi dhidi ya hulka hiyo, iliyokuwa imejichimbia kama utamaduni halisi wa kuendesha uchumi.

Mazingira ya bajeti yalikuwa asilimia 74 ikawa ni matumizi ya kawaida na asilimia 26 matumizi ya maendeleo ambayo Rais John Magufuli, alibadili na kuweka asilimia 39 kuwa ya maendeleo na yale ya shughuli za kawaida kushushwa hadi asilimia 61. Anapoingia madarakani Rais Samia, mabadiliko kidogo yalitokea, matumizi ya maendeleo yalipungua hadi asilimia 37 badala ya 39.

Hatua inayotakiwa hivi sasa ni kufanya kwa ngazi tofauti mabadiliko ya 1986, kwa maana kuwa vitu vilijaa madukani siyo kwa sababu kwa ghafla nchi ilikuwa na tija kiuchumi ila kuwepo uhuru wa kuingiza bidhaa na kuuza bei unayotaka.

Ina maana kuwa vizuizi vya kununua mali, pamoja na kampuni zinazozalisha mali na zenye soko viondolewe, fedha ziingie, mali zinunuliwe, miradi ianzishwe vijana wapate kazi.

**MAKALA**

## TULIKOTOKA, TULIKO & TUNAKOELEKEA...

# Utamaduni wa ndugu kutembeleana ulivyopotea

**Na Adam Fungamwango**

UTAKUMBUKA miaka ya nyuma ndugu, jamaa na marafiki walivyokuwa wakitembeleana majumbani. Tena siyo mtu mmoja, bali familia nzima baba, mke na watuto wawili, watano au zaidi wanaweza kutoka kwao na kwenda kumtembelea ndugu au rafiki. Mara nyingi inakuwa ni siku za mwishoni mwa wiki au wakati wa likizo.

Kuna wale ambao wanawatembea ndugu zao na kukaa kutwa nzima. Wapo wanaokaa siku moja, wenyewe wanaita kulala. Na wapo wanaokaa hata wiki.

Huu ndiyo ulikuwa utamaduni wa Watanzania wengi miaka ya nyuma, na wala haikuonekana kama ni jambo la ajabu. Kwa sababu familia hii itamtembelea huyu na wakati mwingine iliyotembelewa nayo itamtembelea mwenzake wakati mwingine.

Hii ilisababisha upendo, kujaliana, kusaidina na kukuza umoja na mshikamano.

Watu walifahamiana na ndugu wa mbali na karibu, wakaweza kutambuana, na kushibana, tofauti na sasa utashangaa sana kuona watoto wenyewe wa ndugu kwa ndugu hawafahamiani kwa sababu hawajawahi kuonana.

Ikumbukwe kuwa miaka hiyo ninayoisema kabla ya katikati ya miaka ya 1990, kulikuwa hakuna simu za mkononi, hivyo familia moja inaweza kwenda kwa mwingine bila ya mawasiliano yoyote.

Siku zote kwa mtembelewaji kwake inakuwa kama 'sapraizi' tu. Huwa anashtukia tu wageni wamefika. Labda kama walishawahi kukutana na rafiki yake wiki moja au siku chache kabla na kuwambia kuwa siku fulani tunakuja nyumbani.

Kwa sababu hakukuwa na mawasiliano ya simu za mkononi, ilitokea kwa bahati nzuri au mbaya familia hata nne zikakutana kwa mtu mmoja waliyemtembelea.

Uzuri ni kwamba kwa wakati huo, wengi wanaotembelewa huona kama ni baraka kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo wageni wote watapokewa vizuri. Watakula, watalala hadi watakapoondoka, na wala hutosikia lolote, au maneno yoyote kuhusu wao. Huyo aliyetembea inawezekana kabisa baada ya wiki moja naye akamtembelea mwenzake.

Hata wakati wa kufunga shule, watoto wengi wa shule msingi na sekondari wanapofunga, hukuti wakikaa majumbani kwao, wataondoka kwenda kwa ndugu zao kwa karibuni kipindi chote cha likizo.

Kwa sasa haipo hivyo, ni mara chache sana kukuta hali hiyo, wengi wao utawaona wakimalizia likizo zao hapo hapo kwao.

Kwa sasa ni kama utamaduni huo umekufa. Siyo kama hawatembeleani kabisa, lakini ni mara chache sana, kwa sababu maalumu na pia unaweza kukuta baada ya hapo hakukosi vinenoneno.



Nini kimesababisha utamaduni huu kuonekana ni kama unakufa kifo cha asili.

Wengi niliowahoji, walikuwa na maelezo mbalimbali tofauti yaliyosababisha hali hiyo. Ukiyachanganya kwa pamoja, utakuta ni mabadiliko ya maisha, watu na utandawazi.

Wa kwanza aliniambia kuwa teknolojia imechangia sana hali hiyo kwa sababu siku hizi kuna simu za mkononi na mitandao ya kijamii, kama whatsapp, instagram, facebook na mingine mingi ambayo wakati mwingine inasababisha wanandungu, jamaa, marafiki kuunda kundi, ambalo kila siku wanakuwa wanawasiliana, wanabadilishana mawazo, kusaidiana kwa chochote kitakachotokea na kujuliana hali.

Hii imesababisha wengi kutokuwa na sababu ya kutembeleana, hata kwa wanandugu wa kuzaliwa tumbo moja kwa sababu wanajuliana hali kwenye simu au mitandao ya kijamii.

Mwingine akabainisha kuwa mfumo wa maisha ya kijamaa yaliyojengwa na Hayati Baba wa Taifa, Julius Kambarage Nyerere, yalichangia sana watu kutembeleana.

Anasema wakati ule elimu bure, matibabu bure, kazi bwerere kwa mtu ambaye hata wakati mwingine hajamaliza shule alikuwa anaajirika kiasi kwamba, watu walikuwa wanatafutwa kufanya kazi, siyo watu wanatafuta kazi. Kwa sasa akasema maisha ni magumu sana, kumtembelea mtu ni kumpa mzigo wa gharama, kwa sababu maisha ya sasa watu wanaishi kwa bajeti na utaratibu maalumu.

Akaongeza kuwa maisha ya sasa yamekua ya kuchakarika sana ndiyo maana kukutana ndugu ni mara chache sana, labda ni kwenye shuguli za misiba au sherehe.

Yupo mwingine aliyeenda mbali sana akasema kuwa upendo wa wengi umepoa. Utakuta hata wale wanaowapenda ndugu zao na kuwatembelea huonekana kama wanajipendekeza au umasikini ndiyo unaowapeleka kule wanadowea vitu vya wengine.

Kwa sasa anasema inaonekana kabisa binadamu upendo umehamishiwa kwenye fedha na mali. Ni jambo la kawaida mtu kuwa karibu na mali zake kuliko watu.

Watanzania walizidi kutiririka, kwani mama mmoja akasema tatizo la miaka ya sasa mtu anaweza akaenda kwa ndugu yake, lakini sio kwa ajili tu ya kumtembelea, bali kwa lengo maalumu.

Kwa kipindi hiki binadamu wamekuwa wabinafsi sana na kila mtu yupo kivyake, mambo yake na familia yake na ukionekana unaenda kuwatembelea sana ndugu zako, watu wanaona kama unajipendekeza na huna kazi ya kufanya.

Wengine hawataki kabisa, wanasema kwa dunia ya sasa haina muda huo, kama kikao basi kifanywe tu kwenye simu, kama kuonana mtatumiana picha na yoyote mwenye shida, basi watachangishana humo humo kwenye mtandao.

Jamaa mmoja anamalizia kuwa uaminifu umepungua, kwani wakati mwingine huyo huyo anayekutembelea anaweza kukufanyia kisanga hadi ukashangaa. Akaongeza kuwa kwa sasa Watanzania wanaanza kuishi kama Wazungu kila mmoja na familia yake.



## Aliyeopoa miili 25 atishiwa kuawa

**Nairobi,** KENYA

MPIGA mbizi ambaye amekuwa akisaidia kuopoa maiti kutoka Mto Yala, uliopo magharibi mwa Kenya, amejificha baada ya kutishiwa maisha yake.

Taarifa kutoka shirika moja la kutetea haki za binadamu, ilieleza mwanaume huyo ambaye alihusika kuopoa miili ya watu 25 katika kipindi tofauti mwaka jana, alitishiwa kuawa na maofisa wa polisi baada ya kufichua habari hiyo.

Wakati timu ya BBC ilipozuru eneo hilo katika kaunti ya Siaya mwezi uliopita, mzamiaji huyo alieleza jinsi baadhi ya maiti alizoziopoa zikiwa zimefungwa viungo vyao pamoja, huku nyingine zikiwa kwenye magunia.

Wakati huo alisema baadhi ya maofisa wa polisi hawakufurahishwa na hatua ya yeye kuzungumza na wanaharakati wa haki za binadamu na waandishi wa habari kuhusu hali hiyo.

Alitakiwa asizungumze na vyombo vya habari , huku jeshi la polisi likipinga kauli zake, wakisema miili imegunduliwa kwa zaidi ya miaka miwili.

Shirika la Haki Africa lilisema mwanamume huyo sasa ametishwa na polisi.

Mpiga mbizi huyo hivi majuzi aliitwa na polisi, alizuiliwa kwa saa nane na kunyang'anywa simu yake, shirika hilo lilisema katika taarifa yake.

Mkurugenzi wa Haki Afrika, Hussein Khalid, aliiambia BBC kuwa, shirika hilo limeamua kumficha kwa sababu ya wasiwasi wa maisha yake.

Lakini Kamanda wa Kaunti ya Siaya, Michael Muchiri, alisema hakuna sababu ya kuwa na wasiwasi.

Alisema mpiga mbizi huyo alikuwa akifanya kazi vizuri na polisi hawawezi kumtishia mtu ambaye amekuwa akitoa msaada kwao.

Muchiri alisema kati ya miili hiyo iliyopatikana na mpiga mbizi huyo, miwili hadi sasa imetambuliwa kufuatia taarifa za hivi punde na vyombo vya habari.

Katika visa vyote viwili, wanaume hao walikuwa wameripotiwa kutoweka ndani ya miezi mitatu iliyopita - na wote wawili walikuwa wameonekana mara ya mwisho wakiwa hai zaidi ya kilomita 200 kutoka Mto Yala, na kuibua maswali kuhusu jinsi walivyofika huko.

Mashirika ya kutetea haki za binadamu yamehoji iwapo kuna uwezekano wowote wa polisi kuhusika katika vifo hivyo.

Vikosi vya usalama kwa kawaida huwa miongoni mwa washukiwa wa kwanza wakati kunapotokea vifo vinavyotiliwa mashaka na matukio ya kutoweka kwa watu.

Lakini mamlaka husika imewataka wananchi kuacha uvumi huo na kusubiri uchunguzi ukamilike.

Wiki iliyopita, mwanapatholojia mkuu alikamilisha uchunguzi wa miili 17, lakini matokeo bado hayajatolewa hadharani. **BBC**

# Marekani, Urusi zaendelea kutunishiana misuli

**WASHINGTON,** MAREKANI

HALI inazidi kuwa tete katika mpaka wa nchi mbili za Ukraine na Urusi, baada ya kuwepo kwa taarifa za mpango wa uvamizi wa kijeshi.

Tayari Marekani, imeionya Urusi kuachana na mpango wa kuivamia Ukraine na kusisitiza haitakubali kisingizio kitakachoifanya nchi hiyo ndogo kuvamiwa kijeshi.

Taarifa kutoka serikali ya Marekani, ilisema kuwa Urusi imebuni kisingizio cha uwongo kuwalaumu wanajeshi wa Ukraine kwa kuwashambulia watu wanaotaka kujitenga wanaoungwa mkono na Urusi.

Hata hivyo, Urusi ilijibu haraka madai hayo ikisema haina mpango wa opaeresheni bandia ndani ya nchi hiyo ya jirani.

Marekani na Nato wana wasiwasi kufuatia hatua ya vikosi vya Urusi kujikusanya karibu na Ukraine.

Mvutano huo unakuja miaka minane baada ya Urusi kuiteka rasi ya Crimea kusini mwa Ukraine na kuunga mkono uasi wa umwagaji damu katika eneo la mashariki la Donbas.

Maofisa wakuu wa utawala wa Rais Joe Baiden, walisema operesheni hiyo inayodaiwa kupangwa na idara za usalama ya Urusi, kwa kuonyesha picha za majeruhi huko Donbas, ili kuzua hasira dhidi ya mamlaka ya Ukraine.

Mpango huo unaweza kuhusisha kuigiza na kurekodi shambulio la uwongo, walisema viongozi hao.

"Ingeonyesha maiti na maeneo yaliyoharibiwa, vifaa bandia vya kijeshi vya Ukraine, ndege zisizo na rubani zilizotengenezwa Uturuki na waombolezaji wanaoigiza kuzungumza Kirusi," walisema. Lakini maafisa hao walisisitiza kuwa hilo ni chaguo mojawapo tu ambalo Urusi ilikuwa inazingatia, na kuongeza kuwa wanaangalia namna ya kuizuia kufikia hatua iliyokusudiwa.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza Liz Truss, alisema ujasusi wa Marekani ni ushahidi wa wazi na wa kushtua wa uvamizi wa Urusi ambao haukuchochewa na shughuli ya chinichini za kuiyumbisha Ukraine.

"Nia hii mbaya kuelekea nchi huru, ya kidemokrasia haikubaliki kabisa na tunalaani kwa nguvu zote. Uingereza na washirika wetu wataendelea kufichua hila na propaganda za Urusi na kuzikemea," alisema katika taarifa yake.

Msemaji wa Kremlin Dmitry Peskov alijibu ripoti zote mbili akisema hakuna ukweli na kauli hizo zilitolewa tangu nyuma.

Wakati huo huo, Balozi wa Urusi katika Muungano wa Ulaya (EU), Vladimir Chizhov, aliiambia CNN kwamba nchi yake haikupanga operesheni zozote za uwongo za kuivamia Ukraine.

Taarifa za madai ya njama hiyo zinajiri siku moja baada ya Marekani kusema kuwa inatuma wanajeshi zaidi kwa washirika wa Nato barani Ulaya.

Urusi ilisema hatua hiyo ni ya uharibifu na ilionyesha wasiwasi wake kuhusu upanuzi wa Nato Ulaya Mashariki.

Uhasama kati ya mataifa hayo mawili makubwa yanayomiliki silaha za nyuklia duniani, ulianza Vita Baridi kuanzia mwaka 1947 hadi 1989. Wakati huo Ukraine ilikuwa sehemu muhimu ya Muungano wa Kikomunisti wa Kisovieti. **BBC**



Wanajeshi wa Ukraine wakilinda usalama kwa kutumia boti katika mto ambao upo karibu na mpaka wa Urusi jana. Vikosi vya Urusi na Uturuki vinazidi kujiimarisha na kuleta hofu ya kuvamiwa nchi hiyo. **PICHA: THE NEW YORK TIMES**

# Nigeria kuchunguza kampuni 120 kufadhili ugaidi

**ABUJA,** NIGERIA

Nigeria inasema imegundua zaidi ya makampuni 120 na watu 96 wanaohusishwa na ufadhili wa ugaidi.

Waziri wa Habari, Lai Mohammed, alisema watu 45 wanaoshukiwa kufadhili ugaidi wamekamatwa na hivi karibuni watachukuliwa hatua za kisheria.

Alisema shirika la uhalifu wa kifedha la Nigeria, lilipata dola milioni 750 za Kimarekani katika sarafu za ndani na nje zilizohusishwa na ufisadi.

Mwezi uliopita, Tume ya Usalama na Ubadilishanaji wa fedha nchini humo iliongeza uwezo wa mamlaka kufuatilia uhusiano wa kifedha na makundi yanayoshukiwa kuwa ya kijihadi.

Rais Muhammadu Buhari, ambaye sasa yuko katika muhula wake wa pili, alichaguliwa kwa ahadi ya kupambana na ufisadi na kurejesha kiasi kikubwa cha fedha zilizoibwa kutoka Nigeria. **BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## TANGAZO!!
### AFRIWELD INDUSTRIES LTD
### Nafasi ya kazi

Wanahitajika wasichana Wenye umri kuanzia miaka 25-35

**Nafasi:** Mauzo

MSHAHARA wa kuvutia utatolewa!! wahi sasa Kupata nafasi nzuri!!

Kwa mwasiliano zaidi piga simu namba: **0719 184 070**

Piga simu muda wa kazi TU saa MBILI mpaka saa KUMI NA MOJA jioni

**01/01/2022 MPAKA 15/02/2022**

**Asante**

116653602

## KUPOTEA KWA VYETI



**EMERAN BONIFACE RIZIKI,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha NNE na kidato cha SITA, KIDATO cha NNE Chenye index no S.0800/0082 kilichotolewa na baraza la mtihani kupitia shule ya Secondary Loyola Mwaka 2010, KIDATO CHA SITA Chenye index no S.0155/0581 kilichotolewa na baraza la mtihani kupitia shule ya secondary Tabora boys Mwaka 2013, Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi, taarifa ya Polisi **DOD/DOD/RB/600331/2021**

## KUPOTEA KWA CHETI LIVING CERTIFICATE



**SARAH MWAMJENGWA EDSON** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba P0855-0016 kilichotolewa na TARIME TEACHERS COLLEGE CENTRE mwaka 2016. Living Certificate ya Chuo cha TABORA PUBLIC SERVICE COLLEGE pamoja na Transcrip ya Chuo (certificate in records Management) – **TABORA PUBLIC SERVICE COLLEGE.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: TAB/RB/9234/018.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha MAKOLE Mkoa DODOMA**

**Shauri la MADAI Na.10/2022**

**Jina la Mdai MARY KAVINDI**
**Jina la MDAIWA JOSEPH PAULO GYOLY**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)**

Kwa **JOSEPH PAULO GYOLY**
Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba
**MADAI YA TALAKA**
Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 15/02/2022 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo.na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ahili ya kujitetea.
ANGALIZO: kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe 04/02/2022.

**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD & COURT BROKER**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

KWA IDHINI TULOPEWA NA MUHOZA CREDIT LTD TUTAFANYA MNADA WA HADHARA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 05/03/2022 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA GARI AINA YA MITSUBISH PAJERO T 834 CUV. MALI YA SUBIRA MWIJAJEGE KIBONA BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIOKOPA MUHOZA CREDIT LTD. MNADA UTAFANYIKA YADI YA ROYAL RUNNERS DODOMA.MNAKARIBISHWA WOTE.

**KWA MAWASILIANAO TUPIGIE NO. 0712 643 014 au 0713913150**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TANGA**
**Kituo cha….. MJINI TANGA…. Mkoa… TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi…………22…………2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**

**MAREHEMU: MWAJUMA KASSIM, MWANSHAMBA KASSIM NA HADIJA KASSIM**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: MWANANGEMA ATHUMANI SHERIFER**

**TANGAZO**
(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslai yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 22/02/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Imetolewa leo 03/02/2022

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika mahakama ya Mwanzo MAKOLE**
**Usimamizi wa Mirathi NO 10 /2022.**
**Ombi la PETER HOWCENS URIYO Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi Marehemu ROBERT HOWCENS URIYO**
**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII POPOTE ALIPO**
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 04/02/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.
Imetolewa tarehe 27 Mwezi 01 Mwaka 2022.

Sahihi ya Hakimu


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

# HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza, na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao alikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati. Alichojua wengi wanamfuata kama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee. Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani anampenda kwa dhati. Aliyempenda yeye kama yeye na si urembo wake. Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.

# Operesheni Namba Moja-12

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Alijua kabisa kuwa watakuwa wapo hapo muda mrefu na wanamuangalia hatua zote anazozipiga kuelekea kuweka mkoba huo wa pesa, hivyo kukamata bastola kungewafanya wahisi huenda kuna ujanja fulani unataka kufanyika. Na huenda wangemmaliza kabisa.

Aliuweka mkoba taratibu sehemu ambayo alitakiwa auweke. Alisimama kiasi cha nusu dakika kuangalia kama kuna chochote, au kutakuwa na amri yoyote ile, kutoka kwa watu wanaozitaka pesa zile.

Baada ya kuona bado kuna ukimya, alianza kuvuta hatua kadhaa nyuma, baadaye akageuka na kuondoka taratibu sehemu ile ya hatari ambayo aliiona ni sawa na kuwa ndani ya tumbo la nyangumi.

Kila alivyozidi kusonga mbele, ndivyo alivyozidi kuongeza mwendo. Kila hatua aliyopiga alijiona anaingia sehemu salama zaidi kuliko mwanzo.

"Wewee, unakwenda wapi?" Alisikia sauti nyuma yake. Mwili ukafa ganzi. Alijua sasa amekwisha. Akili ya kutaka kuchomoa bastola ikamjia. Alisita kwa sababu hakujua sauti hiyo inatoka wapi na ni nani.

"Simama wewe." Ilikuwa amri. Alijishauri, aitii au asitii.

Akaamua kutii. Lakini akageuza kichwa taratibu ili kujua ni nani.

"Wewe ni nani na unatoka wapi?" Sauti iliuliza.

"Natoka hapo Tazara, nilikwenda kumpokea mgeni, lakini hadi abiria wote wa kwenye treni wanamalizika, sijamuona mgeni wangu." Akaongopa.

Aliyemuona alikuwa ni mlinzi. Ni sare alizovaa zilimtambulisha hivyo. Hakujishughulisha kujua mlinzi huyo analinda, daraja, au moja ya maduka na kampuni yake maeneo yale.

Kitu hicho kilimfaya kushusha presha aliyokuwa nayo. Hata kama atakamatwa na mlinzi huyo kwa kuhisiwa ni mwizi, lakini siyo kama ambavyo angekamatwa na wale majahili ambao waliamuru pesa ziwekwe pale chini ya daraja.

"Huna kitu chochote hapo ulichobeba, maana wengine wezi nyinyi."

"Hapana."

"Haya kimbia upesi, kabla sijakupiga risasi."

Kama kafungwa mota, Jan alitimua mbio ambazo hakupata kukimbia wakati wowote ule wa ujana wake.




**"Sijui, lakini inawezekana ni yule aliyetupa shilingi milioni kumi na tano, Chala ndiye aliyewataarifu." Alijibu, lakini alikuwa anaongopa.**

Wakati anakimbia, masikio yake yote yalikuwa yanategea kama yanaweza kusikia mlio wa risasi kama ambavyo mlinzi yule alimtisha.

Kuna mtu alishawahi kumwambia kuwa akisikia mlio wa risasi basi ajue imemkosa na yupo salama.

"Siku zote kama kuna hatari sehemu watu wabaya wamevamia, ukisikia mlio wa risasi ujue uko hai na uko salama kama hatosikia maumivu. Kwa vyovyote vile, kama risasi ikikupata sawasawa hutoisikia. Kwa sababu utakuwa umeshafariki dunia. Labda iwe imekujeruhi." Alikumbuka maneno ya mtu huyo ambaye kwa haraka haraka alimsahau ni nani.

Mbio zake zilifika ukingoni maeneo ya Buruguni ambapo alivuka barabara na kwenda kwenye kituo cha basi ambacho kilikuwa mkabala na kituo cha mafuta. Alikuwa anatweta, lakini sasa alikuwa na uhakika kuwa hafuatwi na mtu yoyote yule.

Baada ya dakika 10 kupita, basi la Mwananyamala lilifika, ingawa halikuwa na abiria wengi. Alipanda. Alikuwa anarejea nyumbani kwake. Mjomba hakumsubiri kama walivyoongea wenyewe. Waliona ingekuwa hatari kusubiriana. Na waliahidiana mrejesho wa yote yale iwe kesho.

*****************************

"Sasa unasikia. Kwa sababu mmetufanya sisi wajinga, basi kesho saa sita usiku mje pale kuchukua kichwa cha ndugu yenu. Tumechoka kukaa naye. Mwili tutautupa baharini uwe kitoweo cha samaki."

"Hapana, mbona mimi sijawaambia polisi kuhusu suala hili?"

"Kwani aliyepeleka mzigo ule pale ni nani?"

"Ni ndugu yangu."

"Basi inawezekana ndugu yako ndiyo amewaambia polisi suala hili."

"Basi naomba mnisamehe, nipeni nafasi ya mwisho ili nifanikishe."

"Unasikia. Tunakupa nafasi ya mwisho. Kesho kutwa tunazitaka hizo pesa, milioni 50 chini ya daraja la Kajima, lile kubwa la kwanza kama ukitokea Magomeni kwenda Faya. Iwe saa sita usiku. Kumbuka kuwa hili ni onyo la mwisho, vinginevyo tutagawanyisha viungo vya mpwao."

Baada ya jamaa aliyekuwa akiunguruma kukata simu, Ken alibaki na mawazo, huku moyo ukimuenda mbio.

Simu ilivyolia saa moja asubuhi alijua ataambiwa kuwa Diana ameachiwa. Kwa sababu tayari alijua wameshapeleka pesa kiasi kilichopelekwa.

"Ina maana jamaa hawakuchukua ule mzigo. Inavyoonekana wana mkono mrefu sana. Wamejuaje kuwa askari walikuwa wanafuatilia suala hilo?"

Hakuwa na shaka kuwa Jan atafika pale, hivyo hakuwa na haja ya kumpigia simu.

*****************************

"Nani aliyewaambia askari kuwa tunakwenda kuweka mkoba wa pesa chini ya daraja la Mfugale?" Lilikuwa ni swali la kwanza aliloliza mjomba Ken kwa Jan.

"Sijui, lakini inawezekana ni yule aliyetupa shilingi milioni kumi na tano, Chala ndiye aliyewataarifu." Alijibu, lakini alikuwa anaongopa.

Akili yake ilijua kabisa kuwa mtu aliyesababisha askari polisi kujua hilo ni afande Marco ambaye hakutaka kutoa pesa. Akakumbuka maongezi waliyozungumza wakiwa kituoni.

"Mpwa wangu ametekwa na wewe umesikia, wanasema tupeleke kiasi cha shilingi milioni hamsini kwenye daraja la Mfugale pale Tazara, leo usiku saa nane, lakini jamaa wamesema tusiwaambie polisi, vinginevyo watamuua. Usingekuwa mpenzi wake nisingekwambia. Kwa sababu wewe ni polisi, lakini nimelazimika kwa sababu pesa zinatakiwa za kuongezea." Afande Marco alihabarishwa.

"Unasikia kijana, usiwe muoga kiasi hicho, nashukuru kwa taarifa hiyo. We nenda tu nyumbani usiwe na wasiwasi. Ikifika usiku, pelekeni hizo pesa na sisi kama Jeshi la Polisi tutakuja pale na kufanya kazi yetu ya kuwatia nguvuni, halafu watatueleza aliyetekwa nyara yuko wapi."

"Lakini afande mchezo unaotaka kuufanya ni wa hatari kwa Diana." Jan atahadharisha.

"Yule ni mpenzi wangu mimi, nina uhakika hawatomdhuru na mimi hapa ni mkuu na kituo, nawasialiana na wenzangu kufanya jambo hilo." Marco alimhakikishia Jan kuwa watekaji watatiwa nguvuni na Diana ataokolewa.

"Ina maana mzigo bado uko pale pale?" Jan aliuliza.

"Inawezekana au isiwezekane. Nina wasiwasi kama polisi walikwenda pale, wanaweza kuwa wamechukua mzigo huo na kuupeleka kituoni."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# MIPANGO UJENZI WA SANAMU YA NYERERE AU WAKAMILIKA

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

SERIKALI imesema inakamilisha taratibu za ujenzi wa sanamu ya baba wa taifa katika Makao Makuu ya Umoja wa Afrika (AU), jijini Addis Ababa, Ethiopia kwa kushirikiana na familia ya Mwalimu Julius Nyerere.

Akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu (CCM), Asia Halanga, aliyetaka kujua mpango wa serikali kuhakikisha wakandarasi wa Tanzania wanapata fursa ya kujenga mnara wa Mwalimu Nyerere makao makuu ya AU.

Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Pauline Gekul, alisema zabuni Na. SADC / NYERERE ST / 02 ilipotangazwa kati ya Mei na Julai, mwaka 2021 ilitoa fursa sawa kwa wakandarasi wote kutoka nchi wanachama wa SADC.

"Serikali kupitia Baraza la Sanaa la Taifa ilichukua jitihada za kuwatangazia na kuwahamasisha wadau wote nchini kupitia Shirikisho la Sanaa za Ufundi na Idara za Sanaa za Vyuo mbalimbali nchini, ili wenye vigezo vilivyoainishwa kwenye zabuni waweze kuomba kazi hiyo,"alisema.

"Nafahamu wapo wakandarasi wa kitanzania walioomba kazi hii sambamba na wenzao kutoka SADC. Hivi sasa SADC imekamilisha uchambuzi wa nyaraka na muda wowote mshindi atatangazwa baada ya kusaini Mkataba."

Kwa mujibu wa Naibu Waziri huyo, masharti yaliyotolewa na SADC, picha ya Mwalimu Nyerere inayotakiwa kuchorwa ni ya wakati wa harakati za kupigania uhuru, na kwamba wanashirikiana na familia kukamilisha suala hilo.



Kiungo wa Simba, Hassan Dilunga (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi usiku. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mkwasa alia na umaliziaji

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Charles Mkwasa akilia na safu ya ushambuliaji ya timu yake kwa kushindwa kupachika mabao, amekerwa na matokeo ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Mbeya Kwanza katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, jijini Dar es Salaam juzi.

Kocha huyo amesema kama wachezaji wake, hasa safu ya ushambuliaji wangekuwa makini, basi kwenye mechi hiyo wangefunga mabao matatu katika kipindi cha kwanza.

"Hii sare ni kama tumefungwa, tumepata nafasi nyingi tumekosa umakini na ndicho kitu ambacho huwa nakipigia kelele sana mazoezini, nawafundisha kuwa makini na kutulia wakapokuwa wanataka kufunga, lakini kule ni mazoezini, huku ni kwenye mechi unakuta mchezaji hana utulivu, kwa hiyo anakosa bao," alisema Mkwasa.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Mbeya Kwanza, Maka Mwalwisi alisema ameridhishwa na matokeo hayo na kuongeza walicheza na timu ngumu.

"Ruvu Shooting ni timu imara, mechi ilikuwa wazi, tulifanya makosa kipindi cha kwanza wakatufunga. Kipindi cha pili tukarekebisha makosa yetu tukasawazisha. Bado ligi ni ngumu, na haijaisha, nina uhakika tunafanya vyema mbele ya safari," alisema kocha hiyo.

Sare hiyo imeifanya Ruvu Shooting kukaa nafasi ya 14 ikiwa na pointi 12 huku Mbeya Kwanza ikikwea hadi nafasi ya 12 baada ya kufikisha pointi 13, timu zote zimecheza mechi 14.

## DTB FC yapania kuweka rekodi

**Na Adam Fungamwango**

VINARA wa Ligi ya Championship, DTB FC wametamba si tu wanataka kupanda kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, lakini hawataki kupoteza mechi yoyote ile kwenye ligi hiyo msimu huu 2021/22, imefahamika.

Juma Abdul, beki mkongwe na mmoja wa wachezaji mwandamizi wa timu hiyo amesema malengo ambayo wamejiwekea kuanzia viongozi hadi wachezaji ni kuhakikisha wanapanda daraja kwa kishindo.

"Hayo ndiyo malengo ya viongozi, wadhamini wa timu pamoja na sisi wachezaji. Tunataka kupanda mapema sana Ligi Kuu, tena bila kupoteza mechi, kwa hiyo tunawataka mashibiki wetu wajiandae kutupokea," alisema mlinzi huyo wa zamani wa Yanga.

Hata hivyo, Abdul alisema wakati wakijiandaa kupanda, mikakati yao pia ni kuzidi kuikiimarisha kikosi chao kwa ajili ya kukabiliana na ushindani wa Ligi Kuu Bara ambayo msimu huu imekuwa ngumu na timu zinapambana kutafuta matokeo kwa shida.

"Tunataka tukipanda tuwe ni timu tishio na yenye kutoa upinzani mkubwa, hilo tunaliweza kutokana na aina ya wachezaji tulionao, pia tutakapoongeza watu wengine kwenye usajili," Abdul alisema.

## Alliance yaitisha Yanga Princess

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Ilala Queens, Kocha Mkuu wa Alliance Girls, Kassim Juma, amesema kipigo hicho ni salamu kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania dhidi ya Yanga Princess ya jijini Dar es Salaam.

Alliance Girls kutoka Mwanza watakuwa ugenini kukabiliana na Yanga Princess katika mchezo utakaofanyika Februari 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kassim alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanaondoka na pointi sita katika michezo yao miwili watakayocheza hapa jijini Dar es Salaam.

Kassim alisema wamefanikiwa kupata pointi tatu muhimu dhidi ya Ilala Queens na sasa wanajiandaa kuhakikisha wanashinda pia katika mchezo wao unaofuata na kukamilisha malengo waliyojiwekea.

"Tulijiandaa vizuri kupata pointi tatu dhidi ya Ilala Queens, tumerejea tena uwanjani kutafuta alama nyingine dhidi ya Yanga Princess, tunatambua utakuwa mchezo mgumu na wenye ushindani mkubwa," alisema Kassim.

Vinara na mabingwa watetezi wa ligi hiyo ni Simba Queens ya jijini.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**RONALNDO AISUBIRI UNITED**

MSHAMBULIAJI wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, atasubiri hadi Manchester United itakapotangaza utambulisho wa kocha wao mpya kabla ya kuamua ikiwa atasalia hapo Old Trafford. ***(ESPN)***

**ARSENAL KUSAJILI WAPYA**

ARSENAL wanapanga kutumia hadi pauni milioni 180 msimu huu wa joto kumsajili kiungo wa kati wa Wolves na Ureno, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 24, mshambuliaji wa Everton na England, Dominic Calvert-Lewin (24), pamoja na Alexander Isak mwenye miaka 22 kutoka Real Sociedad. ***(Sun)***

**OSIMHEN KUTUA SPURS**

KLABU ya Tottenham Hotspur inapania kumsajili mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen katika msimu wa joto baada ya kumkosa Mnigeria huyo mwenye umri wa miaka 23 ambaye alitemwa na klabu hiyo ya Italia katika dirisha la uhamisho wa Januari. ***(Football Insider)***

**ZANIOLO AWEKWA SOKONI**

KLABU ya AS Roma ipo tayari kupokea ofa za euro milioni 40 kwa ajili ya mshambulizi wa Italia, Nicolo Zaniolo, huku Juventus na Tottenham Hotspur zikiwa miongoni mwa klabu zinazomtaka kiungo huyo wa miaka 22. ***(Calciomercato)***

**NDOMBELE AIWAZA SPURS**

KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Tanguy Ndombele amesema kazi yake Tottenham Hotspur "haijaisha" baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka miaka 25 kurejea Lyon. ***(RMC Sport via Mirror)***

**SALIBA ATAKIWA WEST**

KLABU ya West Ham msimu wa joto inapanga kumsajili beki wa kati wa Arsenal na Ufaransa, William Saliba mwenye umri wa miaka 20, ambaye yuko Marseille kwa mkopo. ***(Jeunes Footeux via Sport Witness)***

**LIVERPOOL YAMTAKA CARVALHO**

LIVERPOOL huenda ikafufufa nia ya kumsaka Fabio Carvalho msimu wa joto baada ya kukaribia kumsajili mshambuliaji huyo wa Fulham mwezi uliopita. ***(AS - in Spanish)***

**ZIDANE MACHO UFARANSA**

KOCHA wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane mwenye umri wa miaka 49 bado hajakubali kuwa mrithi wa Mauricio Pochettino kama kocha wa Paris St-Germain kwa sababu anasubiri kuona ikiwa Didier Deschamps ataachia jukumu lake kama kocha wa Ufaransa. ***(RMC Sport)***

**COSTA AIKATAA FLAMENGO**

WINGA Brazil, Douglas Costa mwenye umri wa miaka 31 amepuuzilia mbali ombi la Flamengo na kukubali kujiunga na klabu ya MLS LA Galaxy kwa mkopo wa miezi sita kutoka Juventus. ***(Fabrizio Romano)***

**BOTMAN ATAJWA SOKONI**

KLABU ya Newcastle itafufua nia yake ya kumsajili mlinzi wa Lille, Sven Botman mwenye umri wamiaka 22 ikiwa itaponea kushushwa daraja kutoka kwenye Ligi Kuu England. ***(Athletic)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NI MISRI VS SENEGAL FAINALI AFCON 2021

Mane, Salah kila mmoja anahitaji kuweka historia katika michuano hiyo...

**YAOUNDE, Cameroon**

GOLIKIPA Gabaski ndiye alikuwa shujaa baada ya kuokoa mikwaju miwili ya penalti na kuisaidia Misri kuwaondoa wenyeji katika michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), Cameroon kwenye mechi iliyofikia hatua hiyo baada ya kutoka suluhu.

Hatua hiyo sasa itazikutanisha Misri na Senegal kwenye fainali itakayochezwa kesho.

Fainali hiyo itawakutanisha washambuliaji wawili wa Liverpool, Mohammed Salah dhidi ya Sadio Mane katika uwanja wa Olembe uliopo katika mji mkuu wa Yaounde

Wenyeji Cameroon walionyesha mchezo mzuri na ari katika dakika tisa za mechi hiyo mara mbili wakigonga mwamba kupitia Ngadeu Ngadjui na shambulizi kali la Samuel Gouet ambalo pia lilipanguliwa.

Nyota wa Misri, Salah alinyamazishwa katika kipidi kirefu cha mechi, akifanikiwa kupiga shambulio moja ambalo halikulenga goli la upinzani.

Lakini hakupiga penalti baada ya wachezaji wa Cameroon kushindwa mara tatu kucheka na wavu, huku Gabaski akiokoa kutoka kwa mkwaju wa Harold Moukoudi na James Siliki naye Clinton N'jie akipiga nje.

Mechi hiyo iliyojawa na ghadhabu katika dakika za lala salama ilimfanya Kocha wa Misri, Carlos Quiroz kulimwa kadi nyekundu kwa kupinga maamuzi ya mwamuzi na wasaidizi, Wael Goma akipewa kadi ya njano.

Hii ina maana makocha wote wawili hawatakuwepo katika fainali, kwani Goma alishalimwa kadi ya njano katika mechi ya robo fainali dhidi ya Morocco.

Wakati huo huo, Cameroon itachuana na Burkina Faso ili kupata mshindi wa tatu katika mechi itakayochezwa leo.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 896

MECHI KALI
BURKINA FASO
VERSUS
CAMEROON
1 | 4.76
X | 3.07
2 | 1.87

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# AUBAMEYANG: ARTETA ALINIONDOA ARSENAL



**BARCELONA, Hispania**

NYOTA mpya wa Barcelona, Pierre-Emerick Aubameyang, amesema tofauti yake na Kocha, Mikel Arteta ndio iliyosababisha yeye kuondoka Arsenal.

Aubameyang aliachiwa kutoka katika mkataba wake pale Arsenal siku ya Jumatatu na kutua Barcelona kwa uhamisho huru.

Na sasa Aubameyang amesema "tofauti" kati yake na Arteta ilichangia uamuzi wake wa kuihama klabu hiyo na kujiunga na Barcelona.

Mshambuliaji huyo wa Gabon alikamilisha uhamisho wa bila malipo kutua Barca siku ya Jumatano baada ya kutupwa nje ya kikosi hicho cha Washikabunduki.

Kuondoka kwa Aubameyang kulikuja muda mchache baada ya kuvuliwa unahodha wa Arsenal kwa utovu wa nidhamu.

"Nadhani ilikuwa shida upande wake tu (Arteta)," alisema nyota huyo mwenye umri wa miaka 32.

"Alifanya uamuzi. Siwezi kusema mengi zaidi. Hakuwa na furaha, japo nilikuwa mtulivu sana lakini ndio hivyo tena."

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Borussia Dortmund, Machi mwaka huu alikosa mechi ya ushindi dhidi ya Tottenham Hotpurs yenye makazi yake Kaskazini mwa London kwa sababu ya "ukiukaji wa itifaki ya kabla ya mechi".

Lakini ana matumaini ya kufufua kiwango chake kule Barcelona kabla ya mechi ya kwanza dhidi ya Atletico Madrid hapo kesho.

"Ni kweli ilikuwa miezi migumu na nadhani soka huwa na mambo haya wakati mwingine," aliongeza Aubameyang.

"Lakini kama itabidi niseme kitu kuhusu mada hii (kuondoka Arsenal), ni sikuwahi kufanya lolote baya kwa upande wangu, lakini nadhani hayo yamepita na ninataka kufikiria kuhusu hali yangu ya sasa."

Aubameyang alifunga mabao 92 katika mechi 163 alizochezea Arsenal baada ya uhamisho wake wa pauni milioni 56 kutoka Dortmund Januari, 2018.

# Pochettino anukia Manchester

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Paris Saint-German, Mauricio Pochettino ananukia kutua katika kikosi cha Manchester United.

United haijapata kocha mkuu wa kumkabidhi timu baada ya kumfuta kazi Ole Gunnar Solskjaer.

Ralf Rangnick anafanya kazi ya muda mfupi ya kuiongoza United, lakini kocha mkuu atakuja mwishoni mwa msimu huu.

Wakati kukiwa na mvutano baina ya mashabiki na wadau wa soka kuhusu nani anafaa kupewa kazi ya kuingoza United, Pochettino na Erik Ten Hag wa Ajax wanahusishwa zaidi.

Kati ya wawili hawa, kuna taarifa zinazosema, Pochettino ana uwezekano mkubwa wa kupewa kazi hiyo kutokana na mwenendo wake ndani ya PSG.

Kwa mujibu wa jarida la France Football, Pochettino hana mahusiano mazuri na wala hapendezwi na namna uongozi wa klabu yake ya sasa unavyofanya naye kazi.

Kwa nje inaonekana kama hana uamuzi na PSG na badala yake, Mkurugenzi wa timu hiyo ndio anaamua kila kitu ndani na nje ya uwanja.

Imeripotiwa kocha huyo hafurahii maisha ndani ya PSG ikiwa ni miezi 13 tu imepita tangu akabidhiwe nafasi hiyo baada ya Thomas Tuchel kuondolewa.

Sababu iliyomwondoa Tuchel PSG ndio hiyo hiyo anayoilalamikia Pochettino kwa sasa.



HABARI MICHEZO


,686,220

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 05/02/22 | 18:00 | Hull City vs Preston | 2.55 | 3.25 | 2.80 |
| 02. 05/02/22 | 18:30 | Maritimo vs GD Estoril | 2.65 | 3.10 | 2.75 |
| 03. 05/02/22 | 19:00 | St Etienne vs Montpellier | 2.57 | 3.31 | 2.67 |
| 04. 05/02/22 | 20:30 | Swansea vs Blackburn | 2.51 | 3.15 | 2.75 |
| 05. 05/02/22 | 21:00 | Pacos Ferreira vs Portimonense | 2.41 | 3.15 | 2.91 |
| 06. 05/02/22 | 23:00 | Twente vs Vitesse Arnhem | 2.33 | 3.20 | 2.95 |
| 07. 06/02/22 | 16:00 | Valencia vs Real Sociedad | 2.70 | 3.20 | 2.65 |
| 08. 06/02/22 | 16:00 | Alanyaspor vs Galatasaray | 2.51 | 3.25 | 2.71 |
| 09. 06/02/22 | 16:00 | Amorebieta vs Real Oviedo | 2.79 | 3.04 | 2.55 |
| 10. 06/02/22 | 17:00 | Sampdoria vs Sassuolo | 2.81 | 3.56 | 2.36 |
| 11. 06/02/22 | 18:15 | Barcelona vs Atletico Madrid | 2.40 | 3.26 | 2.97 |
| 12. 06/02/22 | 20:00 | Udinese vs Torino | 2.86 | 3.21 | 2.51 |
| 13. 06/02/22 | 20:30 | Betis vs Villarreal | 2.33 | 3.44 | 2.94 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 05/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 5888 | Kidderminster vs West Ham | 13.85 | 6.53 | 1.18 |
| 16:00 | 1183 | KMC vs Biashara United | 2.36 | 2.75 | 3.65 |
| 16:00 | 1746 | Kagera Sugar vs Coastal Union | 2.24 | 2.70 | 3.52 |
| 16:00 | 4180 | Elche vs Alaves | 2.41 | 3.15 | 3.05 |
| 16:00 | 5747 | Moroka Swallows FC vs TS Sporting FC | 1.41 | 3.85 | 7.71 |
| 17:00 | 2203 | Roma vs Genoa | 1.34 | 5.18 | 8.16 |
| 17:30 | 2267 | Stuttgart vs Eintracht Frankfurt | 2.69 | 3.48 | 2.47 |
| 17:30 | 2586 | FC Koln vs SC Freiburg | 2.33 | 3.53 | 2.83 |
| 17:30 | 2982 | Augsburg vs Union Berlin | 2.79 | 3.29 | 2.49 |
| 17:30 | 3886 | Mainz vs Hoffenheim | 2.58 | 3.53 | 2.53 |
| 17:30 | 5598 | Arminia Bielefeld vs Monchengladbach | 3.29 | 3.44 | 2.12 |
| 18:00 | 1664 | Southampton vs Coventry | 1.51 | 4.23 | 5.71 |
| 18:00 | 1905 | Stoke City vs Wigan | 1.80 | 3.60 | 4.15 |
| 18:00 | 1927 | Crystal Palace vs Hartlepool | 1.11 | 7.90 | 22.71 |
| 18:00 | 2461 | Manchester City vs Fulham | 1.16 | 7.01 | 13.69 |
| 18:00 | 3004 | Wolverhampton vs Norwich City | 1.62 | 3.80 | 5.14 |
| 18:00 | 3529 | Dundee FC vs Ross County | 2.35 | 3.26 | 2.91 |
| 18:00 | 4314 | Hibernian vs St Mirren | 1.82 | 3.46 | 4.25 |
| 18:00 | 4498 | Livingston vs Aberdeen | 3.20 | 2.96 | 2.36 |
| 18:00 | 4527 | Huddersfield vs Barnsley | 1.66 | 3.69 | 4.92 |
| 18:00 | 5340 | Everton vs Brentford | 2.04 | 3.44 | 3.39 |
| 18:15 | 1517 | Mallorca vs Cadiz CF | 1.82 | 3.41 | 4.62 |
| 18:15 | 4376 | Kortrijk vs St Truiden | 2.29 | 3.40 | 2.91 |
| 18:30 | 1658 | Maritimo vs GD Estoril | 2.65 | 3.10 | 2.75 |
| 18:30 | 3977 | Utrecht vs Cambuur | 1.39 | 4.71 | 6.67 |
| 18:30 | 4363 | Rapid Vienna vs TSV Hartberg | 1.45 | 4.43 | 5.39 |
| 19:00 | 2144 | Fenerbahce vs Basaksehir | 2.18 | 3.34 | 3.15 |
| 19:00 | 3359 | St Etienne vs Montpellier | 2.63 | 3.28 | 2.63 |
| 19:05 | 4913 | HNK Rijeka vs Lokomotiva Zagreb | 1.66 | 3.80 | 4.23 |
| 19:30 | 2678 | Al Ahly Cairo vs CF Monterrey | 6.77 | 4.35 | 1.38 |
| 20:00 | 1158 | Inter vs AC Milan | 1.80 | 3.85 | 4.10 |
| 20:00 | 5326 | Ceske Budejovice vs Sparta Prague | 4.82 | 4.02 | 1.66 |
| 20:30 | 1522 | Cambridge Utd vs Luton Town | 3.30 | 3.45 | 2.08 |
| 20:30 | 2818 | Oostende vs OH Leuven | 2.45 | 3.44 | 2.66 |
| 20:30 | 3443 | Standard Liege vs Cercle Brugge | 2.66 | 3.31 | 2.52 |
| 20:30 | 3644 | Bayern Munchen vs RB Leipzig | 1.40 | 5.19 | 6.39 |
| 20:30 | 4688 | Swansea vs Blackburn | 2.46 | 3.00 | 2.95 |
| 20:30 | 5438 | Celta Vigo vs Rayo Vallecano | 1.93 | 3.41 | 4.01 |
| 20:45 | 4669 | Fortuna Sittard vs Heerenveen | 2.70 | 3.43 | 2.39 |
| 21:00 | 2058 | Burnley vs Watford | 2.22 | 3.25 | 3.30 |
| 22:00 | 2366 | Burkina Faso vs Cameroon | 4.76 | 3.07 | 1.87 |
| 22:00 | 2887 | PSV Eindhoven vs AZ Alkmaar | 1.61 | 3.94 | 4.92 |
| 22:00 | 4409 | PEC Zwolle vs NEC Nijmegen | 2.23 | 3.24 | 3.09 |
| 22:30 | 3829 | Grasshoppers vs FC Zurich | 2.82 | 3.41 | 2.34 |
| 22:45 | 4385 | Fiorentina vs Lazio | 2.37 | 3.46 | 2.86 |
| 22:45 | 5910 | Royal Antwerp vs Union Saint Gilloise | 2.97 | 3.41 | 2.25 |
| 23:00 | 2628 | Monaco vs Lyon | 1.95 | 3.68 | 3.58 |
| 23:00 | 3918 | Tottenham vs Brighton | 1.89 | 3.45 | 3.89 |
| 23:00 | 5134 | Osasuna vs Sevilla FC | 3.46 | 3.16 | 2.20 |
| 23:30 | 5084 | Vitoria Guimaraes vs Sporting Braga | 3.44 | 3.49 | 2.01 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# KOCHA AZAM FC AANZA MAJIGAMBO LIGI IKIKOLEA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Abdilhamid Moallin, amesema limebakia suala la muda katika kuhakikisha malengo yake ya kuifanya timu hiyo kuwa tishio ndani na nje ya mipaka ya Tanzania yanatimia.

Moallin ametua Azam FC akichukua mikoba iliyoachwa na Mzambia George Lwandamina ambaye aliondolewa baada ya timu hiyo kuwa na matokeo yasiyoridhisha.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Moallin alisema ana imani taratibu watu watauona uhalisia wa jambo analolisema baada ya muda mfupi tayari timu yake imeanza kuimarika.

Moallin alisema kikosi chake kitaendelea kuimarika kulingana na mazoezi anayowapa wachezaji wake na siku si nyingi atakuwa na kikosi kinachotoa ushindani.

Aliongeza Azam FC itakuwa tishio katika mechi zitakazofuata lakini pia wanahitaji kufanya vizuri kwenye mashindano ya Kombe la FA na baadaye michuano ya kimataifa.

Alisema licha ya kupitwa pointi 14 na vinara wa Ligi Kuu, Yanga, bado timu yake ina nafasi ya kupambana na kutwaa ubingwa endapo wachezaji watapambana kusaka pointi tatu katika kila mechi watakayocheza na hivyo watafikia malengo.

"Bado tuna nafasi ya kupigania ubingwa, nimeongea na wachezaji wangu na kuwaeleza sisi ni washindi na tunapaswa kuthibitisha hilo, haijalishi utofauti wa pointi ni kubwa kwa kiasi gani, shabaha yetu ni kukusanya pointi katika kila mechi," alisema kocha huyo.

Aliongeza anafurahishwa na kiwango cha wachezaji wake na kwa sasa hakuna timu yoyote inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara au Kombe la FA ambayo inayomuumiza kichwa kwa sababu nyota wake wana uwezo wa kupata matokeo mazuri.



Wachezaji wa Timu ya mpira wa kikapu ya walemavu wakifanya mazoezi kujiandaa na mashindano mbalimbali yajayo kwenye Uwanja wa Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# KMKM, KVZ ngoma uwanjani

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa KMKM, Ame Msimu amesema anatarajia kuwatumia wachezaji wake wapya watatu aliowasajiji hivi karibuni katika mchezo wake wa Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya KVZ utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan, visiwani hapa.

Ame aliwataja wachezaji hao wapya ni pamoja na Mohamed Banka aliyetokea Taifa Jang'ombe, Ali Houmud Balii (Mafunzo) na mchezaji wao waliyemtoa kwa mkopo kutoka Uhamiaji, Ali Jely.

Alisema maandalizi kuelekea mchezo huo yamekamilika na anaamini kikosi chake kitaendelea kutoa dozi na kujiimarisha kileleni.

"Wachezaji hawa wamefanya vizuri katika michezo ya Kombe la ZFF na wamenipa matumaini kuwa watakisaidia kikosi hiki katika michezo ya Ligi Kuu hususani katika mzunguko huu wa lala salama,' alisema Ame.

Kocha huyo aliongeza anatarajia mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu kila timu inahitaji kupata alama tatu ili kujiwekea mazingira kwenye mbio za kutwaa ubingwa wa ligi hiyo.

"Tumejiandaa kushinda, kupata alama tatu ni muhimu sana katika mchezo huu, timu zote zipo katika mbio za ubingwa, hivyo tahadhari kwa wachezaji wa ndani inahitajika sana ili wacheze kwa mipango itakayotupa ushindi," Ame alisema.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Gombani, Pemba ni kati ya Machoamane dhidi ya Mafunzo.

Michezo

Jumamosi Februari 5, 2022

Nipashe



## Ni Misri vs Senegal fainali AFCON 2021



Winga wa Simba, Ousmane Sakho (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa Prisons, Salum Kimenya katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi usiku. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# YANGA SC, MBEYA CITY MAJARIBUNI

●●●Vinara watamba ushindi lazima huku wakikataa kufananishwa...

**Na Saada Akida**

HATUREMBI. Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema timu yake iko imara, kamili na tayari kupambana kupata ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mbeya City itakayochezwa leo usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Nabi alisema maandalizi kuelekea mechi hiyo yamekamilika na wanaupa mchezo huo dhidi ya Mbeya City uzito kutokana na ubora wa timu iliyoko katika nafasi ya tatu kwenye msimamo.

Kocha huyo alisema wachezaji wa Yanga wanatakiwa kuongeza umakini na kucheza kitimu zaidi ili kupata matokeo mazuri na kuendelea kujiimarisha kwenye mbio zao za kutwaa ubingwa wa ligi msimu huu.

"Wachezaji kuingia na kutoka katika kikosi inaweza kuathiri au isiathiri, hii inatokana na majeruhi pamoja na wengine kutumikia adhabu ya kadi, nalazimika kufanya maboreshe katika kikosi changu ili kufikia malengo," alisema Nabi.

Kocha huyo aliongeza ndani ya kikosi chake hakuna mchezaji 'staa', hivyo kurejea kwa Feisal Salum "Feisal Toto" aliyekuwa majeruhi haina maana ataingia moja kwa moja kikosini kwa sababu kila mchezaji Yanga ni bora.

"Yanga hakuna staa, (Fei Toto) amerejea uwanjani na hayuko fiti kwa hali hiyo anatakiwa kufanya mazoezi zaidi na kurejesha kiwango chake ili awe bora zaidi," alisema Nabi .

Alisema kuna kipindi wachezaji wanatakiwa kupata muda wa kupumzika na kumtolea mfano, Dickson Job ametumika katika michezo mingi na juzi akiwa katika mazoezi aliumia, licha ya kutopata maumivu makubwa lakini baada ya uchunguzi ameonyesha anahitaji mapumziko.

"Yanga ni timu kubwa, wote wanapenda mpira na kuheshimu mpira, kwa upande wangu bado sijaridhika na kiwango wanachokionyesha, hadi sasa wana asilimia 65 kufikia malengo, wachezaji wanatakiwa kupambana na kujituma kufikia asilimia hizo zilizobakia," alisema kocha huyo.

Kocha wa makipa wa Mbeya City, Ally Mustafa "Barthez" aliliambia gazeti hili jana wachezaji wote wako fiti na wako tayari kwa ajili ya mchezo huo ingawa watamkosa mchezaji mmoja, Frank Kobela ambaye ni majeruhi.

Nahodha wa Mbeya City, Paul Nonga, alisema: "Tunaenda kupambana kuhakikisha tunapata pointi tatu ili kufikia malengo yetu ya msimu huu ya kumaliza katika nafasi za juu, tunajua mchezo dhidi ya Yanga utakuwa mgumu lakini tunahitaji pointi muhimu na tuko imara kuzipigania alama hizo," alisema Nonga.

## Simba yashusha presha, Morrison akipigwa 'stop'

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuzinduka, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola amesema timu yao ilikuwa bora katika mchezo dhidi ya Prisons na walistahili kupata ushindi kwenye mechi hiyo ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara.

Matola alisema Prisons walicheza mchezo wa kuzuia zaidi katika eneo lao na kuwafanya kuwa wengi hali ambayo iliwapa wakati mgumu kwao kuwapita hasa dakika 45 za kipindi cha kwanza.

Kiungo huyo wa zamani wa mabingwa hao watetezi alisema kipindi cha pili walijaribu kuwafungua na kutengeneza nafasi nyingi ikiwamo ile iliyowapatia penalti na kuzaa bao la ushindi.

"Tulikuwa bora zaidi yao, tulitengeneza nafasi lakini hatukuzitumia vizuri, tulivyorudi kipindi cha pili tulikuwa imara na kufanikiwa kupata ushindi muhimu, ushindi wa leo (juzi), utarudisha morali na hali ya kujiamini kwa wachezaji kutokana kupitia kipindi kigumu katika mechi tatu zilizopita," alisema Matola.

Aliwapongeza wachezaji wake kwa ushindi walioupata kwa sababu ulikuwa mchezo mgumu kutokana na kila timu kuhitaji matokeo ili kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi.

"Huu ulikuwa mchezo muhimu zaidi kwetu tulihitaji pointi tatu ili kuendelea kupunguza wigo wa pointi dhidi ya wanaoongoza ligi ambao wametuacha kwa pointi 10, kupata matokeo imetusaidia kushusha presha," alisema Matola.

Aliongeza kila timu inapokuja kucheza na Simba inafananisha na mchezo wa fainali kwa kutumia nguvu ili kutafuta pointi hali ambayo imejitokeza katika michezo yote waliocheza msimu huu ukiwamo huo wa juzi dhidi ya Prisons.

Wakati huo huo, Simba imetangaza kumsimamisha mshambuliaji wake, Bernard Morrison kwa muda usiojulikana mpaka pale suala lake ya kinidhamu litakapopatiwa ufumbuzi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >